

## **1. UTANGULIZI**

### **1.1 HISTORIA FUPI YA MKOA WA MTWARA**


Mfumo wa utawala wa ukoloni uliigawa Tanzania katika Majimbo 8, Mkoa wa Mtwara ulikuwa ndani ya Jimbo la Kusini ambalo lilijumuisha Mikoa ya Ruvuma, Lindi na Mtwara ambapo Makao Makuu ya Jimbo yalikuwa Lindi.

Mkoa wa Mtwara ulianzishwa rasmi mwaka 1971 kutokana na Mpango wa Madaraka Mikoani ambao ulilenga kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi.

Mkoa huu ulipoanzishwa ulikuwa tayari na Wilaya tatu (3) ambazo ni Masasi iliyoanzishwa mwaka 1928 chini ya ukoloni wa Kijerumani, Newala mwaka 1956 chini ya wakoloni wa Kiingereza na Mtwara ilianzishwa mwaka 1961. Kutokana na ongezeko la watu na kukua kwa Mkoa wa Mtwara ziliongezeka Wilaya nyingine 2 ambazo ni Wilaya ya Tandahimba iliyoanzishwa mwaka 1995 kutoka kwenye Wilaya ya Newala na Nanyumbu ilianzishwa mwaka 2006 kutoka Wilaya ya Masasi.

Kiutawala Mkoa umegawanyika katika Wilaya 5 na Halmashauri 6, Tarafa 25, Kata 149, Vijiji 738, Vitongoji 3,126 na Mitaa 85. Aidha, Mkoa unatarajia kuwa na Halmashauri ya Mji wa Masasi.

**Mchoro Na.1: Ramani ya Mkoa wa Mtwara.**



Takwimu za kiutawala ni kama zinaonyoonekana katika jedwali hapa chini.

**Jedwali Na.1: Takwimu za Kiutawala Mkoa wa Mtwara**

Na.	Halmashauri	Tarafa	Kata	Vijiji	Mitaa	Vitongoji	Idadi ya watu
1	MTWARA MIKINDANI	2	15	6	85	27	126,923
2	MTWARA	6	28	157	0	638	234,563
3	MASASI	5	34	174	0	905	374,139
4	NEWALA	5	28	155	0	471	214,766
5	NANYUMBU	4	14	89	0	504	154,960
6	TANDAHIMBA	3	30	157	0	581	243,885
<b>JUMLA</b>		<b>25</b>	<b>149</b>	<b>738</b>	<b>85</b>	<b>3126</b>	<b>1,349,236</b>

**1.2 MAANA YA NENO MTWARA**

Neno Mtwara limetokana na neno la lugha ya Kimakonde “kutwala” ikiwa na maana ya kuchukua (kunyakua) kitu chochote.

Mtwara ni Jina inalitumika kwa maana 3 tofuati zifuatazo:

- Mtwara jina la Mkoa.
- Mtwara jina la mji wa Makao Makuu ya Mkoa.

- Mtwara ni Wilaya na Makao Makuu ya Wilaya ambayo kiutawala ina Halmashauri 2, ambazo ni Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara/Mikindani na Halmashauri ya Mtwara. Mkoa wa Mtwara una makabila makuu 3 ambayo ni Wamakonde wanaopatikana katika Wilaya za Mtwara, Tandahimba na Newala, Wayao na Wamakua wanaopatikana katika Wilaya za Masasi na Nanyumbu. Kihistoria makabila haya, hapo awali yaliishi pamoja na makabila mengine kaskazini mwa mto Ruvuma. Makabila hayo yaliacha makazi yao na kukimbilia Msumbiji kutokana na uvamizi na vita vya makabila kutoka kaskazini mwa Tanganyika. Katika kuishi Msumbiji matarajio yao ya kuishi kwa amani na utulivu yalitoweka kutokana na kuibuka kwa vita vya Wazulu. Vita hivyo vilisababisha makabila hayo kurudi ng'ambo ya mto Ruvuma yalikuwa zamani. Baada ya kuvuka mto Ruvuma, Wamakonde, Wayao na Wamakua walitafuta maficho hadi kufikia katika bonde la Mkatahumbo na Chitandi. Walitulia katika maeneo hayo na kuondokana na wasiwasi wa kukamatwa na Wazulu.

### **1.3 MAHALI MKOA ULIPO**

Mkoa huu upo Kusini kabisa mwa Tanzania. Kijiografia upo kati ya Longitudo 38° na 40° Mashariki ya Griniwichi, na kati ya Latitudo 10° 05" na 11° 25" kusini ya Ikweta, na una eneo la Kilomita za mraba 16,720 ambayo ni sawa na asilimia 1.9 (1.9%) ya eneo la Tanzania Bara ambalo ni kilomita za mraba 885,987. Takribani asilimia 3.91 (hkt 65,450) ya eneo la Mkoa lipo chini ya hifadhi mbili za wanyama ambazo ni Msanjesi (hkt 44,425) na Lukwika/Lumesule (hkt 21,025).

Mkoa wa Mtwara kwa upande wa Kaskazini umepakana na Mkoa wa Lindi, upande wa Mashariki umepakana na Bahari ya Hindi, upande wa Kusini kuna Mto Ruvuma

unaotenganisha Tanzania na Msumbiji, wakati upande wa Magharibi umepakana na Mkoa wa Ruvuma.

#### **1.4 HALI YA HEWA**

Mkoa wa Mtwara una vipindi viwili vikuu vya majira. Majira ya mvua ambayo huitwa **MASIKA** na majira ya ukavu ambayo huitwa **KIANGAZI**. Hakuna mvua za msimu maalum kama vile za Vuli zinazopatikana sehemu nyingine Tanzania. Kwa kawaida Mkoa wa Mtwara hupata mvua ya wastani wa mm 935 hadi 1,166 kwa mwaka. Wilaya inayoongoza kupata mvua nyingi ni Newala ambayo hupata wastani wa mm.1001, Wilaya inayopata mvua kidogo ni Nanyumbu ambayo hupata wastani wa mm.832.

Kwa kawaida kiwango cha juu cha joto Mkoani Mtwara ni 32C mwezi Disemba na kiwango cha chini cha joto huwa ni 28C mwezi Julai.

#### **1.5 AINA YA UDONGO**

Udongo hutegemea hali ya jiolojia. Katika Mkoa huu kuna kanda mbili za kijiolojia. Kwanza ni ukanda wa pwani ambao unaendelea kwa kilomita 125 kutoka bahari ya Hindi hadi ukanda wa Makonde uliopo Newala. Ukanda huu udongo wake ni wa kichanga na wenye rutuba hafifu na uwezo mdogo wa kushikilia maji. Maeneo mengine katika ukanda huu yana udongo mzito wa aina ya mfinyanzi. Vilevile mawe ya chokaaa yaliyopo pwani hutoa udongo mwekundu unaopitisha maji vizuri.

Ukanda wa pili wa kijiolojia huendelea Magharibi ya ukanda wa pwani, ukanda huu una asili ya mawe yaliojishindilia kwa chini. Kaskazini ya mji wa Masasi kuna udongo wa mfinyanzi

uliochangayika na udongo mwekundu, udongo huu ndio bora kuliko aina zote kwani ndio unaofaa kwa mazao ya chakula na biashara.

### **1.6 WAKAZI WA MKOA WA Mtwara NA SHUGHULI ZAO.**

Shughuli kubwa ya kiuchumi Mkoani Mtwara ni kilimo, ambapo inakadiriwa kuwa 92% ya wakazi wa Mtwara wanajishughulisha na kilimo. Shughuli nyingine muhimu ni uvuvi, ufugaji wa nyuki na viwanda vidogo vidogo. Karibu 85% ya eneo la Mkoa wa Mtwara linafaa kwa kilimo, hata hivyo eneo linalotumika kwa shughuli za kilimo ni chini ya 20%. Jembe la mkono ndio zana kubwa inayotumika katika shughuli za kilimo Mkoani Mtwara, hata hivyo serikali inafanya juhudi kuwawezesha wananchi kutumia zana bora za kilimo kama matrekta makubwa na madogo.

## **2. MUUNDO WA MKOA WA Mtwara ULIVYOBADILIKA KATIKA NYAKATI TOFAUTI KUANZIA 1961**

Baada ya uhuru Mkoa wa Mtwara uliendelea kuwa ni sehemu ya Jimbo la Kusini. Jimbo la Kusini wakati huo lilijumuisha Ruvuma, Lindi na Mtwara likiwa na Wilaya 9 ambazo ni Newala, Masasi, Mtwara, Nachingwea, Lindi, Kilwa, Tunduru, Songea na Mbinga. Kiongozi wa Jimbo alijulikana kama Gavana.

Katika kuhakikisha kuwa huduma za jamii zinasogezwa karibu na wananchi, mwaka 1962 Serikali ilivunja Jimbo la Kusini na kuanzisha Mikoa miwili ya Ruvuma na Mtwara. Mkoa wa Mtwara ulijumuisha eneo la Lindi na Mtwara na Makao yake Makuu yalikuwa Mtwara. Kwa

dhamira ile ile ya kusogeza huduma karibu na wananchi, mwaka 1971 Serikali iliamua kugawanya Mkoa wa Mtwara na kuwa na Mikoa ya Lindi na Mtwara.

Katika kutekeleza dhamira ya Serikali ya kuwapa wananchi madaraka ya kuamua mambo yanayohusu maendeleo yao, mwaka 1971 iliamua kuanzisha mpango wa Madaraka Mikoani. Muundo huo uliendelea hadi kufikia mwaka 1982 ilipoanzisha Serikali za Mitaa na hatimaye mwaka 1997 Serikali ilitunga Sheria Na. 19 iliyounda Sekretarieti za Mikoa zilizoanza rasmi mwaka 1999.

### **3. MAJUKUMU NA MALENGO YA MKOA WA MTWARA**

Dira ya Mkoa ni kuzijengea uwezo serikali za mitaa ili kuziwezesha kujiendesha kwa misingi ya Utawala Bora na kutoa huduma bora kwa wananchi ili kujiletea maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi kwa kushirikiana na wadau wengine. Katika kufikia azma hii Mkoa umejielekeza kutekeleza majukumu yafuatayo;

1. Kutekeleza miradi inayolenga katika kupunguza umaskini hususani miradi ya elimu, afya, maji, barabara na kilimo.
2. Kufuatilia na kuhakikisha kwamba mipango ya maendeleo ya Mkoa na Halmashauri inatekelezwa kwa ukamilifu na malengo yake yanafanikiwa.
3. Kuhakikisha kwamba kunakuwepo na utekelezaji wa sera za kisékta na programu za maendeleo katika Halmashauri.
4. Kuhakikisha kwamba kunakuwepo na utekelezaji wa sera zinazolenga katika kupambana na Ukimwi, vita dhidi ya rushwa, uharibifu wa mazingira na utekelezaji wa maagizo ya Serikali kuu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

5. Kufuatilia na kuhakikisha kwamba kero za wananchi zinaondolewa kwa kufuata sheria, kanuni, taratibu na haki.


#### **4. HALI YA UONGOZI NA UTAWALA KUENZIA 1961**

Kabla ya uhuru, miaka ya mwisho ya ukoloni Wilaya zilikuwa chini ya Mamlaka ya Halmashauri iliyojulikana kama “*Native Authority*”. Baada ya uhuru mfumo wa utawala ulibadilika na kuwa wa Serikali za Mitaa. Katika kipindi cha mwaka 1971-1980 mfumo wa utawala ulibadilika tena na kuwa wa Madaraka Mikoani ukijumuisha Wakuu wa Mikoa ambao walifahamika kama “Regional Commissioner”, Wakuu wa Wilaya ambao walijulikana kama “Area Commissioners”, Afisa Tawala Wilaya au “District Administrative Officer”, Makatibu Tarafa na Makatibu Kata.

Kiutendaji katika ngazi ya Mkoa kulikuwa na Mkurugenzi wa Maendeleo wa Mkoa (Regional Development Director) na Wakuu wa Idara wa Kisekta. Katika ngazi ya Wilaya Mtendaji Mkuu alikuwa ni Mkurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya (District Development Director) akisaidiwa na Wakuu wa Idara wa Kisekta.

Muundo huo uliendelea hadi kufika mwaka 1997 ambapo ulibadilishwa kupitia Sheria Na. 19 iliyounda rasmi Sekretarieti za Mikoa na kubadilisha muundo wa utawala kama ifuatavyo:

**Mchoro Na. 2: Muundo wa Sekretarieti ya Mkoa wa Mwaka 2007.**





Kuanzia mwaka 1961 hadi 2011 Mkoa wa Mtwara uliongozwa na Wakuu wa Mkoa wafuatao:-

**Jedwali Na. 2: Orodha ya Wakuu wa Mkoa wa Mtwara**

<b>Na</b>	<b>Jina</b>	<b>Kipindi/Mwaka</b>
1	Bw. John Nzunda	1962-1972
2	Dr.Wilbert Kleruu	1972-1974
3	Balozi Charles Kileo	1974-1977
4	Lt. Col Kabenga Nsa Kaisi	1978-1980
5	Bw.Lawi Nangwanda Sijaona	1980-1981
6	Bw. Ibrahim Sufian Kajembo	1981-Desemba 1990
7	Col. Ferdinand Swai	Desemba 1990-Februari 1992
8	Bibi Kate Kamba	Februari 1992-Mei 1994
9	Col. Kabenga Nsa Kaisi	Mei 1994-Februari 2003
10	Bw. Isidore Leka Shirima	Februari 2003-Januari 2006
11	Bw.Henry Daffa Shekifu	Februari 2006-Aprili 2007
12	Col.Mst. Anatoli A Tarimo	Mei 2006-hadi sasa

**5. SERA NA SHERIA ZILIZOKUWEPO TANGU UHURU KATIKA MFUMO WA KISIASA, KIULINZI, KIUTAWALA, KIUCHUMI, KITEKNOLOJIA NA KIJAMII**

Mkoa wa Mtwara kama ilivyo Mikoa mingine ya Tanzania ilifuata na kutekeleza sera na sheria mbalimbali zilizotungwa na Taifa, Sera hizo ni pamoja na:-

**5.1 KISIASA**

- Baada ya uhuru siasa iliyokuwepo ni ya ubepari na kulikuwa na mfumo wa vyama vingi vya siasa hadi mwaka 1965 ulipoanzishwa mfumo wa chama kimoja cha Siasa ambacho kilikuwa TANU (Tanganyika African National Union).
- Mwaka 1967 mfumo wa Siasa ya kibepari ulibadilishwa kutokana na kutangazwa kwa Azimio la Arusha ambalo lilianzisha mfumo wa siasa ya Ujamaa na Kujitegemea.

- Mwaka 1992 ulianzishwa mfumo wa vyama vingi vya Siasa, ambapo kwa sasa Mkoa wa Mtwara una vyama 12 vya siasa vifuatavyo:-
  - ✓ Chama Cha Mapinduzi (CCM)
  - ✓ Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA)
  - ✓ Chama cha Wananchi (CUF)
  - ✓ Tanzania Labour Party (TLP)
  - ✓ United Democratic Party (UDP)
  - ✓ APPT Maendeleo
  - ✓ SAU
  - ✓ NCCR-Mageuzi
  - ✓ NLD
  - ✓ Democratic Party (DP)
  - ✓ TADEA
  - ✓ UPDP

## 5.2 KIULINZI

Kiulinzi Mkoa wa Mtwara umetekeleza sera mbalimbali za kiulinzi ambapo Jeshi lililokuwa linaendelea na ulinzi mara baada ya Tanganyika kupata uhuru ni Jeshi la Mfalme wa Uingereza lililojulikana kama (King African Rifle). Jeshi hili liliendelea na kazi ya ulinzi hadi mwaka 1964 lilipoanzishwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) chini ya Amiri Jeshi Mkuu Rais wa kwanza wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere. Majeshi mengine yaliyokuwepo ni pamoja na Jeshi la Polisi kwa ajili ya usalama wa raia na

mali zao, Jeshi la Magereza kwa ajili ya kurekebisha tabia za waharifu, Jeshi la Mgambo kama wasaidizi wa ulinzi wa raia na Ulinzi wa jadi.

Aidha, kutokana na harakati za kudai uhuru wa nchi za Kusini mwa Afrika kama vile Msumbiji, Angola, Zimbabwe na Afrika Kusini. Mkoa wa Mtwara ulikuwa moja kati ya vituo vya mapambano ya ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika.

### **5.3 KIUTAWALA**

Wakati wa uhuru Mkoa ulikuwa na wilaya tatu ambazo ni Masasi, Newala na Mtwara, baadaye Wilaya nyingine mbili ambazo ni Tandahimba 1995 na Nanyumbu 2006 zilianzishwa.

### **5.4 KIUCHUMI**

Kuanzia mwaka 1967 hadi 1991 mfumo wa uchumi wa Taifa ulikuwa ni hodhi ambapo bei za bidhaa zilipangwa na kusimamiwa na Serikali. Aidha, njia kuu za uchumi zilimilikiwa na Umma. Mwaka 1992 mfumo huu wa uchumi ulibadilika kuwa mfumo wa soko huria na sera ya ubinafsishaji ilianzishwa na kutekelezwa.

### **5.5 KITEKNOLOJIA**

Baada ya uhuru teknolojia habari na mawasiliano iliyokuwa inatumika ilikuwa ni ya Analojia na baadaye tuliingia kwenye mfumo wa digitali.

## **5.6 KIJAMII**

Mara baada ya uhuru wananchi waliendelea kuishi kwenye maeneo yao ya asili na mfumo wa mahusiano na Utawala uliongozwa na viongozi wa Kimila. Mkoa wa Mtwara ni kati ya Mikoa ya mwanzo iliyotekeleza kikamilifu Sera ya vijiji ya mwaka 1973 na hatimaye Sera ya vijiji vya Ujamaa ya mwaka 1974. Mnamo mwaka 1975 wananchi wote katika maeneo ya vijijini walikuwa wanaishi katika vijiji vya Ujamaa.

## **6. MABADILIKO NA MATUKIO MAKUU**

### **6.1 MABADILIKO**

#### **6.1.1. KISIASA**

Tangu ulipoanza mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992, chaguzi zote zilizofanyika mwaka 1995 na 2000 nafasi zote za uongozi zilichukuliwa na chama Tawala (Chama Cha Mapinduzi). Katika uchaguzi wa 2000 chama cha TLP kilishinda kiti kimoja cha udiwani Wilaya ya Masasi na 2010 baadhi ya vyama vya siasa vya upinzani vimeweza kupata ushindi wa viti vya vijiji na Udiwani, Chama kinachoongoza kwa upinzani ni Chama cha Wananchi (CUF).

Jedwali lifuatalo linaonyesha matokeo ya uchaguzi mkuu wa 2010 viti vya Udiwani Mkoani Mtwara.

**Jedwali namba 3: Matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa Udiwani Mkoa  
wa Mtwara mwaka 2010**

<b>Jimbo</b>	<b>Idadi ya kata</b>	<b>Chama</b>	<b>Ushindi wa Udiwani kwa Kata</b>	<b>Asilimia</b>
Lulindi	15	CCM	15	100
Masasi	19	CCM	19	100
Nanyumbu	14	CCM	12	85
		CUF	1	7.5
		CHADEMA	1	7.5
Newala	28	CCM	28	100
Tandahimba	30	CCM	21	70
		CUF	9	30
Mtwara Vijijini	28	CCM	26	93
		CUF	2	7
Mtwara Mjini	15	CCM	15	100

## **6.1.2 KIUCHUMI**

### **6.1.2.1 Kilimo**

Shughuli kubwa ya kiuchumi kwa Mkoa wa Mtwara ni kilimo, asilimia 85 ya eneo la Mkoa linafaa kwa kilimo. Uzoefu unaonesha kuwa sehemu kubwa ya wakazi wa Mtwara wanajihusisha na kilimo, ambapo asilimia 86.4 ya wakazi wake hujishughulisha na kilimo cha mazao ya biashara na chakula ambayo ni Korosho, Minazi, Muhogo, Ufuta, Mtama, Mbaazi, Karanga, Mpunga, Choroko, Kunde na Mahindi.

Mkoa umeendelea kufanya jitihada zinazolenga kuhakikisha kwamba wananchi wake wanatumia fursa zilizopo Mkoani, kwa maana ya Ardhi nzuri na yenye rutuba, Hali nzuri ya hewa, Miundombinu ya Barabara na Bandari, Nishati ya gesi na umeme na Uwekezaji ili kujiletea maendeleo kupitia Kilimo cha Mazao mbalimbali ya chakula na biashara, Ufugaji, Ushirika, Maliasili na Uvuvi.

Katika kuhakikisha kuwa kilimo kinaleta tija kwa wananchi na hivyo kuwaletea maendeleo, Mkoa umeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kilimo inayowezesha kuleta mabadiliko ya haraka katika maisha ya wakulima kupitia Sekta ya Kilimo. Mikakati hii imepangwa na inatekelezwa na kila Wilaya kupitia Programu ya Maendeleo ya Kilimo inayojulikana kama ASDP kitaifa au DADPs kwa ngazi za Wilaya.

Maeneo makuu yaliyoainishwa na kupewa kipaumbele ili kuleta mapinduzi hayo ni pamoja na Uimarishaji wa huduma za Ugani, Matumizi ya Zana bora za Kilimo, Uendelezaji wa Kilimo cha Umwagiliaji, Matumizi ya Pembejeo bora za kilimo, Usindikaji wa Mazao ya Kilimo, Uimarishaji wa Ushirika na Masoko ya mazao na Ushirika wa Kuweka na Kukopa.

- **Uimarishaji wa Huduma za Ugani Mkoani.**

Mkoa kwa kushirikiana na Wilaya zake unatekeleza Mfumo wa utoaji huduma za ugani kwa wakulima kupitia Mashamba Darasa ngazi za Vitongoji. Utaratibu huu umewawezesha wakulima ambao kwa muda mrefu hawakupata fursa ya kukutana na Wataalam wa kilimo, kupata fursa hiyo na kujifunza mbinu sahihi za kilimo bora kwa vitendo.

**Picha Na:1 Shamba Darasa La Mihogo Kitongoji Cha Namichi Wilayani Masasi.**



Mashamba darasa yameongezeka kutoka 375 msimu wa 2008/2009 na kuwa 3,105 msimu wa 2010/2011, kwa mchanganuo ufuatao:

**Jedwali Na. 4: Idadi ya Mashamba Darasa kwa kila Halmashauri Mwaka 2008/2009, 2009/2010 na 2010/2011**

<b>Halmashauri</b>	<b>Idadi ya Vitongoji</b>	<b>Idadi ya Vitongoji vyenye mashamba darasa 2008/2009</b>	<b>Idadi ya mashamba darasa 2009/2010</b>	<b>Idadi ya mashamba darasa 2010/2011</b>
Mtwara/Mikindani	35	6	27	35
Mtwara	638	52	618	618
Newala	466	136	466	466
Masaki	905	120	905	893
Tandahimba	589	7	581	589
Nanyumbu	504	54	488	504
<b>Jumla</b>	<b>3,137</b>	<b>375</b>	<b>3,085</b>	<b>3,105</b>

**• Huduma kwa Bwana Shamba/Bibi Shamba kwa Mwaka 2010/2011**

Moja kati ya matatizo yaliyofanya kilimo kukosa tija katika Mkoa wa Mtwara mara baada ya

Uhuru ni uhaba wa Maafisa Ugani na vitendea kazi kwa Maafisa hao na hivyo kufanya

wakulima kutoweza kupata ushauri wa kitaalamu wa kilimo. Mpaka kufikia mwaka 2011 Mkoa wa Mtwara una jumla ya Maafisa Ugani 69 na wote wamepatiwa pikipiki ili kuwafikia wakulima kwa urahisi.

- **Matumizi ya Teknolojia bora za Kilimo.**

Baada ya uhuru zana zilizokuwa zinatumika ni majembe madogo maarufu kwa jina la Chingondola au Mgwilili, Panga na Mundu. Matumizi ya Maksai yalianza mwaka 1980 kwa majaribio katika chuo cha Maendeleo ya Wananchi (FDC) Newala. Kuanzia mwaka 1983 matrekta makubwa yalianza kutumika ambapo ekari moja ililimwa kwa shilingi 45.

Kwa sasa Mkoa unalenga kuongeza matumizi ya zana za kisasa katika kilimo kama matrekta makubwa na madogo ya kusukuma kwa mkono (Power Tillers). Katika kutekeleza azma hii, mwaka 2008/2009 hadi 2010/2011 jumla ya matrekta makubwa **66** na madogo **228** yamenunuliwa na kusambazwa kwa wakulima ambao walichangia asilimia 20 ya gharama za ununuzi kama inavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo.

**Jedwali Na.5: Idadi ya Matrekta Kiwilaya**

Halmashauri	Matrekta Makubwa 2008/2009	Matrekta Madogo	
		Yaliyonunuliwa 2008/2009 -2010/2011.	Eneo lililolimwa 2010/2011 (ekari)
Mtwara/Mikindani	-	6	20
Mtwara	3	41	64
Tandahimba	4	50	43
Newala	9	50	163
Masasi	45	56	165
Nanyumbu	5	25	196
<b>Jumla</b>	<b>66</b>	<b>228</b>	<b>651</b>

Ili kuhakikisha kuwa Matrekta yanafanya kazi na yanadumu, Mkoa unatoa mafunzo kwa madereva (operators), ili wawe na ujuzi wa uendeshaji bora, utunzaji, uunganishaji na urekebishaji wa pembe za majembe na kulima. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, jumla ya



waendesha matrekta 464 wamepewa mafunzo (Mtwara Mikindani 12, Mtwara 78, Newala 100, Masasi 114, Nanyumbu 60 na Tandahimba 100).

**Picha Na: 2 Trekta dogo (Power Tiller)**



• **Matumizi ya Pembejeo bora za Kilimo**

**Pembejeo za Mazao Mchanganyiko.**

Katika msimu wa mwaka 2010/2011 Serikali imetoa ruzuku kwa Mfumo wa Vocha, ambapo jumla ya kaya 24,000 zililengwa kufaidika kwa kupewa mbegu bora, mbolea ya kupandia na mbolea ya kukuzia. Katika Vocha hizo, Serikali ilifidia bei kama ifuatavyo; mbegu ya mahindi (kilo 10) shilingi 10,000, mpunga (kilo 15) 12,000, mbolea ya DAP (kilo 50/Minjingu kilo 100) shilingi 26,000 na UREA imefidiwa kwa shilingi 20,000. Kwa ujumla Serikali imetoa shilingi 1,826,981,000 kwa ajili ya wakulima wa Mkoa wa Mtwara.

**Pembejeo za zao la Korosho**

Kuanzia msimu wa 2007/2008 hadi 2010/2011 Wakulima wa korosho wamepata ruzuku ya pembejeo ya jumla ya shilingi 5,305,430,659.29, kati ya hizo shilingi 4,013,791,067.29

zimetokana na ushuru wa kuuza Korosho ghafi nje ya nchi na shilingi 1,291,639,892.00 zimetokana na bajeti ya Serikali.

- **Hali ya Chakula**

Kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa yaliyosababisha ukame katika miaka ya 1970 na 1980 hali ya chakula Mkoani Mtwara ilikuwa si ya kuridhisha.

Aidha, katika kukabiliana na upungufu wa chakula Mkoa ulianzisha kauli mbiu za kuhimiza wananchi kuzalisha chakula. Kauli mbiu hizo ni kama ONJAMA (Ondoa Njaa Masasi), TUTUMANE (Tuungane Tulime Mazao Newala), KIWAMI (Kilimo kwa Wakazi wa Mjini Mtwara) na KUCHAKUMI (Kujitosheleza kwa Chakula na Kuinua Uchumi Mtwara Vijijini). Kauli mbiu hizi zilisaidia kuhamasisha wananchi kushiriki katika shughuli za kilimo na hivyo kupunguza tatizo la uhaba wa chakula kwa kiasi kikubwa kwa wakati huo.

Takwimu za hali ya chakula kwa mwaka 2011/2012 zinaonyesha kwamba Mkoa utakuwa na ziada ya tani 173,052 za wanga na tani 1,152 za utomwili. Upatikanaji wa chakula kwa sasa unaridhisha. Mavuno kwa ujumla yalikuwa ni mazuri katika Wilaya za Mtwara, Tandahimba, Newala na Nanyumbu. Mavuno ya mazao ya chakula katika Wilaya ya Masasi hayakuwa ya kutosheleza kutokana na upungufu wa mvua katika baadhi ya maeneo.

Mapengo katika maeneo yenye upungufu yatazibwa kutokana na mavuno mazuri ya mazao ya biashara kama Choroko, Ufuta na Karanga. Aidha, wafanyabiashara watasaidia kupeleka chakula katika maeneo yatakayokuwa na upungufu.

**Jedwali Na. 6: Hali ya Chakula Msimu wa 2011/2012 kwa Halmashauri**

Halmashauri	Idadi ya watu (2009)	Mahitaji (Tani)		Mavuno (Tani)		Ziada/upungufu	
		Wanga	Utomwili	Wanga	Utomwili	Wanga	Utomwili
Mtwara/Mikindani	156,436	20,619	10,297	815	650	-19,804	-9,647
Mtwara	217,540	59,715	5,971	82,506	2,827	+22,791	-3144
Tandahimba	204,648	56,602	5,660	99,015	13,322	+94,410	+7662
Newala	198,266	49,208	9,174	83,868	4,546	+34,660	-1,570
Masasi	362,745	108,823	36,275	146,010	40,352	+37,187	+4,080
Nanyumbu	154,960	36,764	14,479	40,572	17,750	+3,808	+3,771
<b>Jumla</b>	<b>1,294,595</b>	<b>331,731</b>	<b>81,856</b>	<b>452,786</b>	<b>79,447</b>	<b>+173,052</b>	<b>+1,152</b>

- **Mazao ya Biashara na Chakula**

**Mazao ya Biashara**

Wakati uhuru unapatikana mwaka 1961 mazao ya biashara katika Mkoa wa Mtwara yalikuwa ni korosho, pamba, ufuta, karanga, nyonyo na nazi. Mnamo mwaka 1970 kilimo cha zao la Pamba kilipigwa marufuku ili kuzuia uwezekano wa Funza Wekundu (Red Bollworm) kusambaa katika mikoa ya kaskazini kutokea nchi ya Msumbiji.

Mwaka 1981 zao la Soya liliingizwa mkoani na kulimwa kwa wingi zaidi katika Wilaya ya Newala, zao hili liliingizwa Mkoa wa Mtwara kufuatia juhudi za Afisa Kilimo wa Wilaya ya Newala Ndugu Mwakaniche. Mpaka kufikia mwaka 2011 Mkoa wa Mtwara umekuwa na mazao ya biashara kama Korosho, Choroko, Ufuta, Karanga, Njugu na Nazi

**Mazao ya chakula**

Mazao yaliyokuwa yanalimwa ni pamoja na mtama, muhogo, njugu, uwele, ulezi, mpunga, mbaazi, mahindi na kunde. Mpaka kufikia mwaka 2011 Mkoa wa Mtwara umekuwa na mazao

ya chakula kama choroko, mahindi, mtama, Mpunga, ulezi, uwele na mboga za jamii ya mikunde.

- **Mifugo**

Kabla ya uhuru wananchi wa Mkoa wa Mtwara walijihusisha na ufugaji wa mifugo midogo midogo kama vile kuku, bata, njiwa na mbuzi. Kuanzia mwaka 1980 wananchi hao walianza ufugaji wa ng'ombe wa asili hasa katika Wilaya ya Masasi.

**Picha Na: 3 Ng'ombe wa asili Wilayani Masasi**



Kutokana na kuongezeka kwa mwamko wa matumizi ya mazao ya mifugo idadi ya baadhi ya mifugo imeongezeka huku mingine ikipungua Mkoani Mtwara kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:-

### Jedwali Na 7: Idadi ya Mifugo

Aina ya Mifugo	Mwaka 1996	Mwaka 2011
Ng'ombe	19,700	24,294
Mbuzi/Kondoo	16,400	590,152
Nguruwe	6,000	9,420
Kuku/Bata/Kanga	3,200,000	1,297,730
<b>JUMLA</b>	<b>3,239,100</b>	<b>1,913,118</b>

#### 6.1.2.2 Uvuvi

Shughuli nyingine za kiuchumi zinazofanywa na wananchi wa Mkoa wa Mtwara ni pamoja na uvuvi katika bahari ya Hindi. Aidha, uvuvi pia upo kwenye mito, maziwa na mabwawa kama ifuatavyo:- Mto Ruvuma wenye urefu wa kilomita 500, Ziwa Chidya kilomita za Mraba 1.5, Ziwa Kitere Kilomita za mraba 1.5 na Mabwawa 112 ya kufugia samaki katika Halmashauri za Wilaya za Masasi 6, Newala 5, Nanyumbu 5, Mtwara 80 na Mtwara/Mikindani 16. Aina ya samaki wanaopatika ni pamoja na Changu, Tasi, Kolekole, Kibua, Nguru, Pweza na Kamba (Prawns).

#### 6.1.2.3 Biashara

##### Soko la mazao ya biashara

Katika miaka ya 1961 hadi 1973 mazao ya biashara yaliyozalishwa na wakulima Mkoani Mtwara yalikuwa yakinunuliwa kwa mfumo wa wanunuzi binafsi. Halmashauri kama ya Newala ilijenga masoko ya kuuzia mazao kwa kila Tarafa, ambapo wakulima walikusanya mazao yao na kuyauza kwa wanunuzi ambao waliyasafirisha na kuyauza kwa wanunuzi wakuu wa Kihindi Mtwara mjini.

Serikali baada ya kuona kuwa mkulima hanufaiki na mazao anayolima iliamua kuanzisha Taasisi za ununuzi wa mazao hayo. Taasisi hizo ni GAPEX, NMC na CATA.

Hata hivyo katika miaka ya 1990 Serikali ilijiondoa katika masuala ya biashara na shughuli za ununuzi wa mazao kufanywa chini ya mfumo wa soko huria. Hali ya soko la mazao ya biashara limeendelea kuwa huria hadi mwaka 2007/2008 Mkoa ulipoanza kutekeleza Sheria Na. 10 ya mwaka 2005 ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani hasa kwa zao la korosho. Mfumo wa Stakabadhi Ghalani ni mfumo ambao unawataka wakulima wa korosho kupeleka mazao yao kwenye Vyama vya Msingi vya Ushirika kisha vyama hivyo kupeleka kwenye maghala makuu kwa ajili ya mnada.

#### **6.1.2.4 Viwanda/Ushirika**

Baada ya Uhuru mpaka kufikia mwaka 1970 Mkoa wa Mtwara ulikuwa na viwanda vidogo vya jamii vilivyokuwa vikijihusisha na shughuli kama Uhunzi na Upasuaji wa mbao.

Kuanzia mwaka 1980 Serikali iliweka mkazo katika kuhamasisha wananchi kuanzisha viwanda vidogo vidogo chini ya usimamizi wa Shirika la kuendeleza Viwanda Vidogo (SIDO), viwanda hivyo vilijihusisha na utengenezaji wa vifaa vya chuma, uchongaji wa samani na bidhaa nyingine zitokanazo na mbao.

Serikali pia ilianzisha kiwanda cha kutengeneza Ngalawa eneo la Mikindani chini ya usimamizi wa (TAFICO). Aidha kulianzishwa kiwanda cha Mkonge Kabisera na cha

usindikaji wa ndimu maeneo ya Kilombero na Mahurunga ambavyo vilikufa kutokana na kukosekana kwa mali ghafi.

**Picha Na 4: Kiwanda cha kutengeneza Ngalawa Mikindani**



Aidha Serikali kupitia Mamlaka ya Korosho ilianzisha viwanda (5) vya ubanguaji wa Korosho katika maeneo ya Mtwara, Newala na Masasi. Hata hivyo kutokana na kupanda kwa bei ya korosho ghafi, na kushuka kwa uzalishaji wa korosho baada ya wananchi kuiacha mikorosho yao na kuhamia katika vijiji vya ujamaa, viwanda vilikosa malighafi na hivyo kusababisha kufungwa kwa viwanda hivyo.

**Usindikaji (ubanguaji) wa korosho**

Pamoja na kuuzwa kwa wingi korosho nje ya nchi mkulima aliendelea kuwa katika hali duni kiuchumi, kwani mfumo wa kuuza korosho ghafi ulikuwa wa kinyonyaji. Kutokana na hali hiyo Uongozi wa Mkoa uliamua kuandaa utaratibu utakaowezesha mkulima kupata bei nzuri ya korosho yake kwa kufanya yafuatayo:-

1. Kuimarisha utaratibu wa mauzo ya korosho kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani. Mfumo huu umesaidia mkulima kupata bei nzuri kutoka shilingi 300 kwa kilo mwaka 2005/2006 hadi shilingi 1,900 kwa kilo mwaka 2010/2011.
2. Kuhamasisha wananchi kuanzisha vikundi vya ubanguaji wa korosho (Semi processing).
3. Kuzihamasisha Halmashauri na Vyama Vikuu vya Ushirika (TANECU na MAMCU) kuanzisha viwanda vya kukausha, kumenya kudarajisha na kufungasha, ambapo vikundi vya wakulima vitapeleka korosho zilizobanguliwa kwa hatua za awali (Semi Processed cashewnuts) kwa ajili ya ukamilishaji na uuzaji wa korosho hizo kwenye soko la kitaifa na kimataifa.

Kupitia utaratibu huu mkulima atauza korosho zake kwa bei ya soko la kimataifa na kukatwa gharama za kukausha, kumenya, udarajishaji, ufungashaji na mauzo.

Hali ya ubanguaji wa korosho hadi mwaka 2011 ni 20 - 25% sawa na tani 25,000 – 30,000 kupitia viwanda vikubwa (OLAM na AGROFOCUS), vya kati (River Valley Foods Co Ltd, Kitama Farmers Group Co. Ltd, Masasi High Quality Farmers Product Ltd) na vikundi vya wakulima, ambapo kuna vikundi 150 vya wakulima (Masasi 6, Tandahimba 7, Mtwara 13, Newala 120, Nanyumbu 3 na Mtwara Mikindani 1). Vikundi hivi vinabangua korosho zinazoliwa ndani ya nchi.



**Picha Na: 5 Kiwanda cha kubangua Korosho Kitama.**



**6.1.2.5 Madini**

Mkoa wa Mtwara una aina mbalimbali za madini yakiwemo madini ya mawe ya bahari (Coral stones) na vito. Mawe ya bahari huchimbwa kando ya bahari ili kuzalisha chokaa ambayo hutumika katika ujenzi wa nyumba na vito kama vile Sapphire, Red Garnets, Marble, Alexandrite, Christabella na Rhodelite yanayopatikana Wilayani Masasi, Newala, Tandahimba na Nanyumbu. Aidha, Mkoa unayo gesi asilia inayopatikana kwenye eneo la Ghuba ya Mnazi katika Wilaya Mtwara

Mwaka 1996 jumla ya wachimbaji wadogo 21 waliruhusiwa kuchimba madini ya vito mkoani Mtwara na mpaka kufikia mwaka 1997 jumla ya maduka 21 yanayoshughulika na ununuzi na uuzaji wa vito yalikuwa yamefunguliwa na gramu 50,514.11 za vito zenye thamani ya shililngi 113,164,600 zilikuwa zimenunuliwa mkoani Mtwara.

### Jedwali Na.8 Aina za Madini Mkoani Mtwara, 1997

<b>Wilaya</b>	<b>Madini</b>
Newala	Rhodolite, Sapphire, Amethyst na Red Garnets
Tandahimba	Sapphire, Tourmaline, Red Garnets na Graphite
Masasi	Red Garnets, Sapphire, Marble, Chrysoberl, Alexandrite, Tourmaline na Rhodolite

#### 6.1.2.6 Misitu/Nyuki/Mazingira

Mkoa wa Mtwara una hifadhi ya misitu yenye jumla ya hekta 140,000 na Misitu Matajiwazi zaidi ya hekta 300,000. Aina ya miti inayopatikana katika maeneo mbali mbali ya mkoa wa Mtwara ni pamoja na Mivule, Misufi pori, Mitumbati, Mbambakofi, Mipingo, Mbalamwezi, Pangapanga, Paurosa na aina nyingine za miti ya mapambo na matunda.

Mazao ya misitu yanayopatikana katika mkoa wa Mtwara ni pamoja Mkaa, Kuni, Majengo, Kamba, Mbao, Asali, Nta na dawa za asili. Katika jitihada za kuhifadhi mazingira Mkoa wa Mtwara umekuwa na Programu mbali mbali za kuhifadhi mazingira kupitia Halmashauri za Wilaya. Kupitia Programu Shirikishi ya Utunzaji wa Misitu (PFM) jamii katika vijiji inashiriki katika utunzaji wa misitu. Misitu hii huwasaidia wananchi kuongeza kipato kupitia uuzaji wa mbao na Ufugaji wa nyuki.

#### 6.1.2.7 Wanyamapori

Mkoa una Mapori mawili ya akiba ya Wanyamapori ambayo ni Lukwika/Lumesule lenye ukubwa wa kilometa za mraba 220.25 na Msanjesi lenye ukubwa wa kilometa za mraba 444.25. Mapori haya yana wanyama na ndege wa aina mbalimbali. Katika mto Ruvuma

unaokatisha Halmashauri zote za Mkoa kuna Viboko na Mamba. Askari wa Wanyamapori wameendelea kufanya doria katika maeneo yote ya Mapori ya akiba ikiwa ni sehemu ya ulinzi wa kila siku wa watu na mali zao dhidi ya wanyama wakali na waharibifu kama vile Tembo, Nyati, Simba na Mamba wanaojitokeza kwenye makazi ya watu na kwenye mashamba ya mazao ya Chakula na Biashara.

- **Utalii**

Mkoa wa Mtwara una vivutio vya utalii kama sehemu ya kihistoria ya Mikindani ambapo ilikuwa ni soko la watumwa na gofu la nyumba aliyoishi Dr. David Livingstone. Pia ina Fukwe zenye mchanga mweupe za Ruvula (Msimbati), Shangani na Msanga Mkuu. Boma la Kijerumani lenye Handaki - Newala, Bonde la Mto Ruvuma na hifadhi za mikoko, Shimo la Mungu-Newala, Miinuko ya Makonde-Newala, misitu ya Miyuyu – Newala, hifadhi za Lukwika/Lumesule na Msanjesi, Ngoma za asili, Vinyago na historia ya makabila.

### **6.1.3 Kiulinzi**

Baada ya kupata Uhuru mwaka 1961 hadi 1964 kiulinzi, tuliendelea kuwa chini ya jeshi la Mwingereza lililojulikana kama KAR (King's African Rifles). Mnamo mwaka 1964 Jeshi la Wananchi wa Tanzania lilianzishwa na Amiri Jeshi Mkuu akiwa ni Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

### **6.1.4 Kiutawala**

Kiutawala, wakati wa uhuru kulikuwa na Serikali Kuu na Mamlaka za Wenyeji (Native Authorities) ambapo katika ngazi ya Mkoa kulikuwa na Wakuu wa Majimbo (Provincial

Commissioners) na Wilayani kulikuwa na uongozi wa Mamlaka za Wenyeji (Native Authorities). Katika ngazi za Vijiji kulikuwa na Akida, Liwali na Jumbe.

#### **6.1.5 Kiteknolojia/Mawasiliano.**

Kabla ya uhuru wananchi wa Mtwara walikuwa na magazeti yafuatayo *Uchele* (Newala) lenye maana ya Kumekucha kwa lugha ya Kimakonde, *Ipipi* (Masasi) lenye maana ya giza kwa lugha ya Kimakua, *Katapala* (Mtwara Vijijini) lenye maana ya pendeza kwa lugha ya Kimakonde na *Hekanelo* (Mtwara Mjini) lenye maana ya Cheka leo kwa lugha ya Kimakonde. Baada ya uhuru Mkoa wa Mtwara uliendelea kuwa katika nyanja ya mawasiliano kupitia Shirika la Utangazaji la Tanganyika (TBC).

Mpaka miaka ya 2009 redio zilianza kuongezeka Mkoani Mtwara na kufikia jumla ya vituo 4. Vituo 4 vya binafsi ambavyo ni Redio Maria, Pride FM, INFO Radio na SAFARI Radio. Mkoa una kituo 1 cha televisheni kinachomilikiwa na Halmashauri ya wilaya ya Masasi na kingine kimoja kinachotarajiwa kufunguliwa wilayani Newala.

Hadi mwaka 1995 huduma za simu kwa Mkoa wa Mtwara zilikuwa zikitolewa na kampuni ya TTCL tu, lakini kwa sasa kampuni 5 za simu zinatoa huduma zake kwa mkoa wa Mtwara. Kampuni hizo ni TTCL, Vodacom, Tigo, Airtel na Zantel.

Kwa upande wa huduma za mtandao wa Internet, hadi mwaka 1995 huduma hiyo haikuwepo Mkoani Mtwara. Huduma hii ilianza rasmi mwaka 2004 ambapo Mkoa uliunganishwa na

ulimwengu kupitia Makondenet na kampuni ya simu ya TTCL na sasa unajengwa mkongo wa Taifa kwa ajili ya kuboresha mawasiliano.

## **6.1.6 KIJAMI**

### **6.1.6.1 ELIMU**

Sekta ya elimu Mkoani Mtwara imepata mafanikio katika kipindi cha miaka 50 ya Uhuru 1961 – 2011. Taasisi za utoaji huduma ya elimu kwa jamii kama vile shule za Awali, Msingi, Sekondari, na Vyuozimeongezeka katika vipindi mbalimbali.

**Picha Na.6: Shule ya Sekondari Rahaleo Mtwara/Mikindani**



Mabadiliko katika sekta ya elimu yamejitokeza kama ifuatavyo:

#### **A: Kipindi cha kuanzia mwaka 1961 – 1996**

- Shule za Awali zilikuwa 117
- Shule za Msingi zilikuwa 493

- Shule za Sekondari za Kidato cha I - IV zilikuwa 13
- Shule za Sekondari za Kidato cha V - VI ilikuwa 1
- Vyuo vya Ualimu vilikuwa 3
- Chuo Kikuu kimoja (1)
- Wanafunzi walioandikishwa Darasa la I – VII walikuwa 141,167
- Wanafunzi walioandikishwa Kidato cha I – VI walikuwa 4,305
- Walimu wa shule za Msingi walikuwa 1,191
- Walimu wa shule za Sekondari walikuwa 242
- Madawati yalikuwepo 35,089
- Nyumba za walimu wa shule za Msingi zilikuwa 563
- Vyumba vya madarasa vilikuwa 1,156

**B: Kipindi cha kuanzia mwaka 1997 – 2011**

- Shule za Awali zipo 562
- Shule za Msingi zipo 626
- Shule za Sekondari za Kidato cha I - IV zipo 137
- Shule za Sekondari za Kidato cha V - VI zipo tisa (9)
- Vyuo vya Ualimu vipo vinne (4)
- Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) kimoja (1)
- Vyuo Vikuu vipo viwili (2)
- Wanafunzi walioandikishwa Darasa la I – VII ni 244,240
- Wanafunzi walioandikishwa Kidato cha I – VI ni 42,965

- Walimu wa shule za Msingi wapo 4,950
- Walimu wa shule za Sekondari wapo 1,187
- Madawati yapo 71,192
- Nyumba za walimu katika shule za Msingi zipo 1,542
- Vyumba vya madarasa katika shule za Msingi vipo 3,794

Jedwali lifuatalo linaonesha mafanikio katika sekta ya elimu mkoani Mtwara.

Jedwali Na.9: Mafanikio ya sekta ya Elimu kwa mwaka 1961-2011

Mwaka 1961-1996		Mwaka 1997-2011		Ongezeko	%
Taasisi	Idadi	Taasisi	Idadi		
Shule za Awali	117	Shule za Awali	562	445	480
Shule za Msingi	493	Shule za Msingi	626	133	27
Shule za Sekondari i-iv	13	Shule za Sekondari i-iv	137	124	95
	1	Shule Sekondari v-vi	9	8	800
Shule Sekondari v-vi	3	Vyuo vya Ualimu	4	1	33
Vyuo vya Ualimu	0	Vyuo vya Ufundi (VETA)	1	1	100
Vyuo vya Ufundi (VETA)	1	Vyuo Vikuu	2	1	50
Vyuo Vikuu	141,167	Uandikishaji wanafunzi darasa i-vii	244240	103073	73
Uandikishaji wanafunzi darasa i-vii	4,305	Uandikishaji wanafunzi kidato i-iv	42965	38660	896
Uandikishaji wanafunzi kidato i-iv	1191	Walimu wa shule za Msingi	4950	3759	315
	242	Walimu wa Sekondari			
Walimu wa shule za Msingi	35089	Madawati	1187	939	388
Walimu wa Sekondari	563	Nyumba za Walimu Msingi	71192	36103	103
Madawati	1156	Vyumba vya madarasa	1542	979	174
Nyumba za Walimu Msingi			3794	2638	228
Vyumba vya madarasa					



### **6.1.6.2 AFYA**

Afya ni kati ya huduma muhimu sana kwa binadamu. Wakati wa ukoloni Wananchi wa Mkoa wa Mtwara walikuwa na huduma za afya kupitia waganga wa jadi na zahahati chache zilizojengwa na wakoloni.

Kwa kuwa huduma za afya za kisasa zilikuwa zinapatikana mijini na maeneo ya Wamisionari, waliofaidika ni wananchi wachache waliokubali kujiunga na madhehebu mapya ya dini na ambao walikuwa wanaishi karibu na huduma hizo. Aidha, watumishi wachache wa maofisini ambao walikuwa wanatumikia Serikali za Wakoloni ndio waliofaidika na huduma hizo. Wananchi walio wengi vijijini waliendelea kuishi bila huduma ya afya ya uhakika.

Wakati wa utawala wa kikoloni wa Kiingereza, wakoloni hao walianza kuona umuhimu wa afya za wananchi kwa manufaa ya wakoloni wenyewe. Jukumu la kusimamia na kuwapatia wananchi vijijini huduma ilikabidhiwa Serikali za Kienyeji (Native Authorities). Kwa kuwa Serikali hizi hazikuwa na uwezo mkubwa, huduma iliyopatikana vijijini ilikuwa duni sana upande wa madawa, wafanyakazi na vifaa vya kazi na ilitofautiana sana kutoka eneo moja hadi jingine na huduma iliyokuwa inapatikana ni tiba tu.

Japokuwa Wakoloni na Wamisionari walileta huduma za afya za kisasa, kulikuwa na dosari nyingi ambazo baada ya uhuru Serikali imejitahidi sana kurekebisha. Baadhi ya dosari hizo ni;

- Huduma za afya hazikupewa umuhimu unaostahili kama ilivyo sasa.
- Wananchi waliendelea kuwa na imani na Waganga wa Jadi.

- Huduma za afya zilikuwa zinapatikana mijini tu na sehemu maalum, vijijini kuliachwa bila huduma.
- Wakoloni walitilia mkazo katika huduma za tiba pekee. Huduma za kinga hazikuwepo kabisa, ambapo baada ya uhuru mkazo ulitiwa kwenye huduma za kinga.
- Huduma zilitolewa kwa matabaka.
- Ushirikishwaji wa wahudumiwa haukuwepo.
- Baada ya uhuru wakazi wa Mkoa wa Mtwara wapatao 800,000 walipata huduma za afya kupitia Hospitali 5, (3 za Serikali 1 kwa kila Wilaya na hospitali 2 za madhehebu za dini Ndanda na Mwena). Mwena ilikuwa ni hospitali ya wagonjwa wa ukoma.

Kwa upande wa huduma za Vijijini hadi kufikia mwaka 1982 Mkoa ulikuwa na jumla ya vituo vya afya 9 (vitatu kila Wilaya). Kwa upande wa zahanati Mkoa ulikuwa na jumla ya zahanati 105, kati ya hizo 97 za Serikali na 8 za Madhehebu ya dini.

Sehemu hizi za tiba zilizotajwa ziliendelea kutoa huduma za tiba na kinga katika Mkoa wa Mtwara, dhidi ya matatizo makuu ya afya ambayo yalikuwa ni Malaria, kuharisha na kutapika, ukoma, surua, pneumonia, utapiamlo, kifua kikuu, kichocho, magonjwa ya watoto wachanga pamoja na kuzaliwa kabla ya wakati, upungufu wa damu na mengineyo.

Jitihada za kufikisha huduma za kinga na tiba vijijini zilifanikiwa japokuwa kulikuwa na changamoto kadhaa kubwa ikiwa ni uwiano wa vituo hivi vya tiba. Vijiji ambavyo vilikuwa mbali na zahanati au vituo vya afya vilipatiwa huduma za mwanzo (First aid boxes). Kutokana na matatizo makubwa ya kiafya ya Mkoa wa Mtwara mkazo zaidi uliwekwa katika huduma za kinga; maana matatizo yaliyo mengi yanaweza kukabiliwa kwa kuyakinga.

Aidha mkazo mkubwa uliwekwa katika kufungua kliniki za akina mama wajawazito na watoto wadogo katika zahanati zisizo na kliniki ili kuwawezesha akina mama wajawazito na watoto wadogo kuchanjwa dawa za kuzuia magonjwa ya kuambukiza, kuwagundua mapema watoto wenye matatizo ya utapiamlo, kutoa elimu ya afya kama vile elimu ya chakula na lishe, uzazi wa majira na kutibu shida ndogo ndogo.

Kutokana na utaratibu huu kila zahanati ilitarajiwa kuendelea kutoa huduma za tiba na kinga kwa wananchi wote waliopo Vijijini. Pamoja na jitihada za Serikali kufikisha huduma za tiba na kinga Vijijini, jitihada hizi zilikuwamishwa na matatizo matatu yafuatayo:

- Upungufu wa watumishi. Ijapokuwa zilikuwepo zahanati nyingi na vituo vya afya bado havikuweza kutoa huduma kwa ukamilifu kutokana na upungufu wa wahudumu, waganga na wakunga. Kwa hiyo ililazimika sehemu zingine kutofungua kliniki za watoto wadogo.
- Upungufu wa zana za kazi uliophelekea upungufu wa utoaji wa huduma kikamilifu.
- Uhaba wa fedha za kugharamia utoaji huduma. Kwa kuwa vifungu vilivyotolewa vilikuwa vidogo sana, wakati vifaa na madawa yaliendelea kupanda bei, matokeo yake ni kushindikana kupata mahitaji ya kutosha kwa utoaji wa huduma Vijijini.

Mpaka kufikia mwaka 2011 huduma za afya Mkoani Mtwara zimeboreshwa kwa kiwango kikubwa kama ifuatavyo:-

- ✓ Hospitali 5 (Serikali 4 na binafsi 1).
- ✓ Vituo vya afya viko 15 na kati hivyo vituo 12 ni vya Serikali wakati 3 ni vya watu binafsi

- ✓ Zahanati ziko 160, za Serikali 133 na za watu binafsi ni 27.
- ✓ Idadi ya madaktari bingwa wapo Wanne (4) ambao wapo katika Hospitali binafsi.
- ✓ Idadi ya madaktari 25
- ✓ Matabibu wasaidizi meno 3
- ✓ Madaktari wasaidizi 54
- ✓ Idadi ya Matabibu 153

### **6.1.6.3 HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII:**

Huduma za Idara ya Ustawi wa Jamii Mkoani Mtwara zilianza mapema mwaka 1970, wakati huo zilikuwepo ofisi mbili ambazo ni Ofisi ya Ustawi wa Jamii Mkoa na Ofisi ya Ustawi wa Jamii Wilaya ya Masasi. Huduma zilianza kuimarika kuanzia mwaka 1999 mara baada ya kuanzishwa kwa Sekretarieti ya Mkoa. Katika kipindi cha miaka 12 ( 1999 hadi 2011) ofisi 4 mpya za Ustawi wa Jamii zilifunguliwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa za Newala, Tandahimba, Manispaa ya Mtwara na Halmashauri ya wilaya ya Mtwara.

Huduma za Ustawi wa Jamii zinatolewa katika maeneo Makuu manne ambayo ni: - Huduma kwa Watu wenye Ulemavu na wazee.

- Huduma kwa Familia na Watoto.
- Huduma za Vituo vya kulea watoto wadogo mchana
- Huduma za kisheria kwa Watoto na Vijana ( Juvenile Justice)

- **Huduma kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi (MVC)**

Katika miaka ya uhuru wa Tanzania, Mkoani Mtwara tatizo la watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi halikuwa kubwa, tatizo hili limejitokeza katika miaka ya 1990 na

kushamiri zaidi katika miaka ya 2000. Sababu zinazochangia kuwepo kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira hatarishi:

- ✓ Uyatima unaotokana na watoto kupoteza wazazi ikiwa ni athari za janga la UKIMWI.
- ✓ Utelekezaji wa watoto unaofanywa na wazazi wasiowajibika (Child neglect)
- ✓ Watoto kuzaliwa nje ya ndoa.
- ✓ Mila na desturi ya mfumo wa Familia ambapo mkuu wa kaya/familia kuwa mwanamke/mama (Matrimonial system), hali hii ipo zaidi katika wilaya za Masasi na Nanyumbu.
- ✓ Umaskini wa kipato miongoni mwa wazazi hasa wa mjini.

- **Utambuzi watoto wanaoishi katika Mazingira Hatarishi:**

Kutokana na ushirikiano wa karibu baina ya Wadau wa watoto wanaoishi katika Mazingira Hatarishi (Serikali kuu, Mamlaka za serikali za Mitaa mkoani Mtwara na Mashirika ya kimataifa ambayo ni Pact Tanzania na UNICEF), mwaka 2008 na 2009 kulifanyanyika zoezi la kuwatambua watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi. Kwa mujibu wa zoezi hilo, Mkoa una jumla ya watoto 16,364 wanaoishi katika mazingira hatarishi. Jedwali lifuatalo linaonesha mgawanyo wa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi kiwilaya Mkoani Mtwara.

**Jedwali Na. 10: Mgawanyo wa Idadi ya Watoto wanaoishi Katika mazingira hatarishi  
katika Halmashauri za Mkoa wa Mtwara.**

<b>Na.</b>	<b>Halmashauri ya Wilaya</b>	<b>Mwaka wa Utambuzi wa watoto</b>	<b>Idadi ya MVC</b>
1.	Mtwara/Mikindani	2008	1,277
2.	Mtwara (V)	2009	2,073
3.	Tandahimba	2009	5,400
4.	Newala	2009	1,104
5.	Masasi	2009	4,615
6.	Nanyumbu	2008	1,895
		<b>Jumla kuu</b>	<b>16,364</b>

Baada ya kutambua idadi ya watoto na mahitaji yao, Wadau hao pia wanaendelea kushirikiana katika kuwahudumia watoto hao kwa kuwapatia mahitaji muhimu yafuatayo:-

- ✓ Chakula
- ✓ Mavazi
- ✓ Matibabu
- ✓ Elimu
- ✓ Malazi
- ✓ Ushauri wa kisheria
- ✓ Huduma za kisaikolojia na kijamii (Psychosocial Support.)

- **Huduma kwa watu wenye ulemavu**

Kuanzia mwaka 1961, Mkoa wa Mtwara haukuwa na takwimu zozote za watu wenye Ulemavu. Kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya kitaifa ya Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2003, Mkoa wa Mtwara mwaka 2011 unakadiriwa kuwa na watu wenye ulemavu wapatao 130,000. Mkoa kwa kushirikiana na wadau wengine, umekuwa mstari wa mbele katika kuwahudumia Watu wenye ulemavu.

#### **6.1.6.4 HUDUMA ZA MAJI**

Maji ni hitaji kubwa na la muhimu katika mwili ya binadamu. Inakadiriwa kuwa robo tatu ya mwili wa binadamu ni maji. Maji pia ni muhimu sana katika maisha na shughuli mbali mbali za maendeleo ya binadamu. Maji hutumika katika shughuli mbalimbali za kijamii kama matumizi ya nyumbani na hata kiuchumi kama matumizi ya maji viwandani na katika shughuli za kilimo na umwagiliaji.

Makazi mengi ya watu duniani huanzishwa karibu na vyanzo vya maji na hii hutokana na umuhimu wa maji kwa maisha ya binadamu. Aidha Mkoani Mtwara miji ama makazi ya mwanzo ya wenyeji wa Mkoa huu yalianzishwa karibu na vyanzo vya maji. Miji hii midogo kama Mikindani ulioanzishwa karibu na Mchuchu mahali ambapo kuna chemchemi za maji safi na salama, Masasi na Newala ambapo wakazi wake waliweka makazi katika bonde la Makonde ambalo lina chemchemi za kudumu.

Kadri idadi ya watu inavyoongezeka ndipo mahitaji na matumizi ya maji huongezeka, na kadri idadi ya watu inavyozidi ndivyo shughuli za binadamu zinavyoongezeka na kuathiri mazingira na vyanzo vya maji. Hii ndio sababu iliyopelekea kuhitajika kwa mbinu mbadala zitakazoweza kuwapatia wakazi maji safi na salama.

Kabla ya Uhuru na hata baada ya uhuru kumekuwepo miradi mbali mbali ya maji. Katika mpango wa usambazaji wa maji Vijijini mwaka 1958 mradi wa kwanza wa maji wa Nanyamba wilayani Mtwara ulianzishwa. Wilayani Masasi hata kabla ya uhuru kulikuwa na miradi minne (4) ya maji na kupanuliwa zaidi baada ya Uhuru ambapo Vijiji vingi zaidi vilifaidika na miradi

hiyo hasa mradi wa maji Lulindi. Wilayani Newala mradi wa kwanza wa maji ulikuwa chini ya uongozi wa kikoloni wa Mwingereza ulikuwa ukitoa maji toka katika kisima kilichochimbwa chini ya mteremko wa uwanda wa juu wa Makonde Mashariki na kusambazwa mjini Newala. Mradi huo ulijulikana kwa jina la Shirika la Maji la Makonde (Makonde Water Corporation). Hata hivyo baada ya uhuru jina la mradi huo lilibadilishwa na kuitwa Makonde Water Supply.

✓ **Ugavi wa maji vijijini**

Aina za vyombo vya ugavi wa maji Vijijini hutofautiana kati ya Wilaya na Wilaya. Kwa Wilaya ya Mtwara Vijijini kuna maji ya bomba, visima virefu, malambo na visima vifupi, kwa upande wa Masasi kuna visima vifupi na Newala hutegemea maji ya bomba ambayo husukumwa kwa nguvu ya umeme.

Jedwali lifuatalo linaonyesha mgawanyo, aina na idadi ya vyombo vya ugavi wa maji Kiwilaya mkoani Mtwara hadi mwaka 2011 (Takwimu za wilaya ya Newala zinajumuisha wilaya ya Tandahimba)

**Jedwali Na. 11. Mgawanyo, aina na Idadi ya vyombo vya Ugavi Maji Vijijini**

<b>Wilaya</b>	<b>Visima Virefu</b>	<b>Visima Vifupi</b>	<b>Malambo</b>
Mtwara Vijijini	71	368	10
Masasi	44	44	4
Newala	16	16	0
Nanyumbu	75	53	6
Tandahimba	12	26	4
Mtwara Mikindani	3	34	0
<b>JUMLA</b>	221	541	24

**Ugavi wa maji mijini**



- ✓ Hadi mwaka 1996 Mji wa Masasi ulikuwa unategemea vyanzo vinne vya maji. Vyanzo hivyo vilikuwa ni lambo la Mchema, visima virefu 5, visima vifupi 50 na maji ya chemchemi ya Mwena na Mwiti. Vyanzo vikuu vya maji kwa mji wa Mtwara/Mikindani vilikuwa ni visima virefu 9. Mji wa Newala ulikuwa unahudumiwa na mradi wa maji ya bomba uliokuwa ukitumia umeme. Mpaka mwaka 2003 bodi za Mamlaka za Maji nne zilianzishwa ambazo ni MTUWASA mwaka 1996 (Mtwara), Mamlaka ya Maji Mjini Masasi mwaka 2003, Mamlaka ya Maji ya Uwanda wa Makonde mwaka 2003 na Mamlaka ya maji Mangaka 2008.

## **6.2 MATUKIO MAKUU**

### **6.2.1 Kisiasa**

- ✓ Rais wa Awamu ya Tatu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa anatoka Mkoani Mtwara.
- ✓ Maadhimisho ya Sabasaba kitaifa yalifanyika Mtwara mwaka 1982.
- ✓ Ziara ya Rais mstaafu wa Marekani Bw. Bill Clinton mwaka 2010.

### **6.2.2 Kiutawala**

- ✓ Kugawanyika kwa jimbo la kusini 1962 na kuanzishwa kwa Mikoa ya Mtwara na Ruvuma.
- ✓ Kugawanyika kwa Mkoa wa Mtwara mwaka 1971 na kuanzishwa Mkoa wa Lindi na Mtwara.

### **6.2.3 Kiulinzi**

- ✓ Mkoa wa Mtwara ulikuwa ngome ya wapigania Uhuru wa nchi za Kusini mwa Afrika.

- ✓ Kurejeshwa kwa mabaki ya Mashujaa kutoka Msumbiji na kuzikwa upya katika eneo la Mashujaa la Naliendele mwaka 2004.

#### **6.2.4 Kijamii**

- ✓ Kuzuka kwa ugonjwa wa Ndui mwaka 1967.
- ✓ Mafuriko makubwa ya mwaka 1990 yaliyoharibu miundombinu ya mawasiliano.
- ✓ Kuzama kwa kivuko cha mto Ruvuma kwenye kijiji cha Kilambo.
- ✓ Uzinduzi wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MEM) ulifanyika Mkoani Mtwara mwaka 2004.

#### **6.2.5 Kiuchumi**

- ✓ Kuanzishwa kwa safari za anga za kampuni ya Precision Air 2009 na Fly 540 mwaka 2011.
- ✓ Kufanyika kwa maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani Kitaifa mwaka 2009.

### **7. MAFANIKIO YALIYOPATIKANA MPAKA SASA**

#### **7.1 HUDUMA ZA JAMII**

##### **7.1.1 ELIMU**

**Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 50 ya Uhuru 1961 hadi 2011.**

- ✓ Ongezeko la Shule za awali 445 toka 117 hadi 562.
- ✓ Ongezeko la shule za Msingi 133 toka 493 hadi 626.
- ✓ Ongezeko la Shule za Sekondari 124 zenye kidato cha I hadi IV toka 13 hadi 137.
- ✓ Ongezeko la shule za Sekondari 8 zenye kidato cha V hadi VI toka 1 hadi 9.

- ✓ Ongezeko la Chuo 1 cha Ualimu toka 3 hadi 4.
- ✓ Kuanzishwa kwa Chuo kimoja cha VETA.
- ✓ Ongezeko la Chuo Kikuu 1 kutoka 1 hadi 2.
- ✓ Ongezeko la Uandikishaji wa Wanafunzi 103,073 wa Shule za Msingi kutoka 141,167 hadi 244,240.
- ✓ Ongezeko la uandikishaji wa Wanafunzi 38,660 wa Shule za Sekondari toka 4,305 hadi 42,965.
- ✓ Ongezeko la Walimu 3759 wa shule za Msingi toka 1191 hadi 4950.
- ✓ Ongezeko la Walimu 939 wa shule za Sekondari toka 242 hadi 1,187.
- ✓ Ongezeko la madawati 36103 toka 35,089 hadi 71,192.
- ✓ Ongezeko la vyumba vya madarasa 2638 toka 1156 hadi 3794.
- ✓ Ongezeko la nyumba za Walimu 979 toka 563 hadi 1542.

### **7.1.2 AFYA**

Hadi kufikia mwaka 2011 sekta ya afya imeimalika kama ifuatavyo:-

- ✓ Hospitali 5 (Serikali 4 binafsi 1).
- ✓ Vituo vya afya viko 15 na kati hivyo vituo 12 ni vya serikali wakati 3 ni vya watu binafsi
- ✓ Zahanati ziko 160 za serikali 133 na za watu binafsi ni 27.
- ✓ Idadi ya madaktari bingwa 4
- ✓ Idadi ya madaktari 25
- ✓ Matabibu wasaidizi meno 3

- ✓ Madaktari Wasaidizi 54
- ✓ Idadi ya Matabibu 153

### **7.1.3 MAPAMBANO DHIDI YA UKIMWI**

- ✓ Kiwango cha maambukizi kimkoa kimeshuka toka 7% mwaka 2003/2004 mpaka 3.6% mwaka 2007/2008.
- ✓ Huduma ya kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto wakati wa ujauzito, kujifungua na wakati wa kunyonyesha zinatolewa katika Hospitali zote, Vituo vya afya na Zahanati.
- ✓ Mkoa una jumla ya Vituo 178 vinavyotoa huduma za Afya za VVU/UKIMWI.
- ✓ Waratibu na Waelimishaji Rika 31 kutoka Sekretarieti ya Mkoa wamepatiwa mafunzo juu ya Mpango wa kudhibiti maambukizo ya VVU/UKIMWI sehemu za kazi.
- ✓ Sekretarieti ya Mkoa inaendelea kutoa huduma ya chakula cha ziada na lishe kwa watumishi 5 waliojitokeza wenye VVU.
- ✓ Hospitali ya Mkoa na hospitali za Wilaya zote zimeanzisha Mpango wa kudhibiti maambukizo ya VVU/UKIMWI katika maeneo yao ya kazi.
- ✓ Halmashauri zote zimeunda kamati za mapamano dhidi ya ukimwi kuanzia ngazi ya kijiji, kata na wilaya. (VMAC, WMAC, CMAC) Kazi kubwa za kamati hizi ni kusimamia / kuratibu shughuli za mapambano dhidi ya UKIMWI.
- ✓ Jumla ya chupa 16,543 za damu katika mpango wa Damu salama zimekusanywa na kati ya hizo chupa 12,711 zimesanbazwa katika hospitali 16 Mkoani Mtwara.
- ✓ Jumla ya Asasi zisizo za Kiserikali 189 zinazojishughulisha na mapambano dhidi ya UKIMWI zimeanzishwa.

- ✓ Huduma ya dawa za kupunguza makali ya UKIMWI inatolewa katika vituo 33 vya huduma za afya.
- ✓ Kuna jumla ya vituo 83 vya kudumu vya Ushauri Nasaha na Wanasihhi 120 wamepatiwa mafunzo rasmi ya unasihhi.

#### **7.1.4 Huduma za Ustawi wa Jamii**

- ✓ Kuanzishwa kwa Matawi 5 ya Vyama vya watu wenye Ulemavu ambavyo ni CHAWATA, CHAVITA, TLB, Chama cha Wenye Mtindio wa Ubongo na SHIVYAWATA
- ✓ Viongozi wote wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu wamepatiwa mafunzo ya Ujasiriamali (2010).
- ✓ Chama cha TLB kimepatiwa msaada wa mradi wa mashine ya kusagisha nafaka toka kwa Katibu Tawala wa Mkoa.
- ✓ Mkoa una shule 2 maalum kwa ajili ya watoto wenye ulemavu, shule hizo ni Lukuledi (wenye Ulemavu wa Kusikia) na Lulindi(Mtindio wa Ubongo) wilayani Masasi.
- ✓ Kuanzishwa kwa vitengo 6 vya elimu maalum kwa watoto wenye ulemavu wa akili katika shule za msingi zifuatazo:-
  - 1) Luchingu – Newala
  - 2) Ndanda - Masasi
  - 3) Mji Mpya – Tandahimba
  - 4) Shangani – Mtwara/Mikindani
  - 5) Mtandi – Masasi

#### 6) Rahaleo- Mtwara/Mikindani

- ✓ Kuimarika kwa mahusiano baina ya wananchi na jamii ya Watu wenye Ulemavu (Hakuna kesi yeyote ya mauaji ya Albino katika Mkoa wa Mtwara).
- ✓ Utambuzi wa watoto 16,364 wanaoishi katika mazingira hatarishi na mahitaji yao.
- ✓ Jumla ya Watoto 800 walio katika mazingira hatarishi wanapatiwa misaada ya kielimu.
- ✓ Viongozi wa jamii na watendaji wa Kata 157 kati yao 102 kutoka Wilaya ya Tandahimba na 55 kutoka Manispaa ya Mtwara Mikindani wamepatiwa mafunzo ya **PARA SOCIAL WORKERS** ili wasaidie kutoa huduma za Ustawi wa jamii katika vijiji na mitaa.
- ✓ Kituo kimoja cha kutunzia wazee wasiojiweza Mkoani Mtwara kimeanzashiwa katika kijiji cha Mkaseka Wilayani Masasi.
- ✓ Asasi 4 za Wazee zimeanzishwa wilani Newala, Masasi, Mtwara na Mtwara-Mikindani.
- ✓ Hospitali zote za Serikali zimeanzisha utoaji wa huduma bure kwa wazee (Dirisha maalumu kwa ajili ya Wazee)
- ✓ Kuanzishwa kwa Chuo kimoja cha watu wenye ulemavu wa Macho (Wasioona) kilichopo Mtapika-Masasi.

#### 7.1.5 MAJI

- **Maji Mijini, Vijijini na Miji Midogo**

- ✓ Bodi za Mamlaka ya maji nne zilianzishwa . MTUWASA mwaka 1996, Mamlaka ya Maji Mjini Masasi na ya Uwanda wa Makonde mwaka 2003 na Mamlaka ya Maji Mangaka mwaka 2008.
- ✓ Mpaka mwaka 2011 jumla ya Visima vifupi 541 vimechimbwa.
- ✓ Mpaka mwaka 2011 jumla ya Visima virefu 221 vimechimbwa.
- ✓ Jumla ya Malambo 24 yamechimbwa hadi kufikia mwaka 2011.

#### 7.1.6 MAENDELEO YA JAMII

- **Vikundi vya uzalishaji mali vya wanawake**

Mkoa una jumla ya vikundi vya uzalishaji mali vya wanawake 2,039 vyenye wanachama 18,542. Vikundi hivi vinajihusisha na shughuli zifuatazo; kilimo cha mazao ya biashara na chakula, ufugaji, ushonaji, ususi, kilimo cha mboga, utandaji samaki, mgahawa, Mama Lishe na Biashara ndogo.

##### **Jedwali Na.12 Vikundi vya Uzalishaji Mali vya Wanawake hadi Juni 2011**

<b>Halmashauri</b>	<b>Idadi ya vikundi vya uzalishaji mali</b>	<b>Idadi ya wanachama</b>
Mtwara-Mikindani	244	1,220
Mtwara	362	7,240
T'himba	610	3,340
Newala	572	3,420
Nanyumbu	151	1,722
Masaki	320	1,600
<b>JUMLA</b>	<b>2,039</b>	<b>18,542</b>

- **Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kuanzia**

Mwaka 2004 Mkoa ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi 73,985,000.00 kwa vikundi vya uzalishaji mali vya wanawake 149 kutoka serikali kuu na Halmashauri

zilitoa mikopo ya thamani ya shilingi 174,958,100.00 kwa vikundi 515. Kuanzia 2005-2010, jumla ya shilingi **176, 077,849.00** zilikopeshwa katika vikundi vya kiuchumi **335**

**Jedwali Na. 13: Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kuanzia 2005-2010**

<b>Halmashauri</b>	<b>Kiasi cha Mkopo</b>	<b>Idadi ya vikundi vilivyokopeshwa</b>
MtwaraMik	21,950,000	32
Mtwara	66,422,454	69
Newala	58,080,000	105
Masasi	48,451,395	60
Tandahimba	25,454,000	39
Nanyumbu	15,500,000	30
<b>Jumla</b>	<b>176,077,849</b>	<b>335</b>

✓ **Uendelezaji wa vituo vya kulelea watoto (Day Care Centers)**

Mwak 2004 Mkoa ulikuwa na jumla ya vituo vya kulelea watoto 48 vilivyokuwa na jumla ya watoto 4,520 .Hadi kufikia mwaka 2011 Mkoa umekuwa na vituo vya kulelea watoto 83 vyenye jumla ya watoto 7225 ambavyo ni sawa na ongezeko la vituo 35 sawa na ongezeko la 73%.

**7.1.7 MAENDELEO YA VIJANA**

- ✓ Mkoa una jumla ya vikundi 440 vyenye wanachama 3050 (wanaume 2392, wanawake 958).
- ✓ Vituo 54 vya uelimishaji rika vya vijana vimeanzishwa mkoani Mtwara kama ifuatavyo: Masasi 22, Nanyumbu 12, tandahimba 2, Mtwara Vijijini 18.
- ✓ Kumla ya mitandao 5 ya Vijana imeanzishwa mkoani Mtwara kama ifuavyo: Masasi (MASAYODEN), Tandahimba (TAYODEN), Newala (NEYONE), Mtwara Vijijini (MTWAYODEN) na Nanyumbu (NAYODEN).



- ✓ Uanzishwaji wa Asasi zisizokuwa za Kiserikali zinazoshughulika na masuala ya Vijana.

#### **7.1.8 UTEKELEZAJI WA SHERIA ZA KAZI NA KANUNI ZAKE**

- ✓ Kuwepo kwa Mabaraza ya wafanyakazi katika Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- ✓ Kuanzishwa kwa kamati za kukuza ajira katika Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- ✓ Jumla ya watumishi 34 wa Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara wamepata mafunzo juu ya Sheria za kazi na Kanuni zake.

#### **7.1.9 MICHEZO NA UTAMADUNI**

- **Michezo**

Kuanzishwa kwa Vyama vya Michezo vya MTWAREFA kwa ajili ya mpira wa miguu na CHANEMTWA kwa ajili ya mpira wa pete.

- Mkoa wa Mtwara unafanya vizuri katika ya UMITASHUMTA na UMISSETA ambapo mwaka 2000 ulikuwa Mshindi wa kwanza Kitaifa kwa Mpira wa Miguu katika Michezo ya UMITASHUMTA.
- Kuanzishwa kwa Shirika la SDA (Sports Development Aid) ambalo linasaidia katika kuendeleza Michezo katika shule za Msingi na Sekondari. Kila mwaka Shirika hili hupeleka timu ya Wanafunzi nchini Finland kushiriki mashindano ya mpira wa Miguu.

- Kila kijiji kina kiwanja cha michezo.
- Maafisa 3 wa michezo toka Tandahimba, Newala na Mtwara wamepatiwa mafunzo ya uongozi wa michezo mwaka 2008.
- **Utamaduni**
  - ✓ Mkoa una jumla ya vikundi vya Sanaa 211.
  - ✓ Mkoa umehifadhi maeneo ya kihistoria ya Maboma ya Wajerumani Newala na Mikindani.
  - ✓ Tangu 2007 Mkoa unafanya Tamasha la utamaduni lijulikanalo kama MAKUYA.

## 7.2 SEKTA YA UZALISHAJI

### 7.2.1 Kilimo

- **Uzalishaji wa mazao ya Chakula**

Uzalishaji wa mahindi umeongezeka kutoka tani 58,830 msimu wa mwaka 2005/2006 hadi tani 67, 945 mwaka 2011 sawa na ongezeko la tani 9,115 sawa na 86.6%. Hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula ipo kama ifuatavyo:

**Jedwali Na 14: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula Kimsimu**

Mazao ya Chakula	2005/2006	2006/2007	2007/2008	2008/2009	2009/2010	2010/2011
Muhogo	353157	390784	417147	366557	495499	510014
Mahindi	58830	49093	57067	31423	69922	67945
Mpunga	19958	27205	32632	24652	42751	48281
Mikunde	16710	14001	17481	18835	22481	24115
Mtama	31547	29108	42882	22129	37940	46276

- **Uzalishaji wa Mazao ya Biashara**

Uzalishaji wa mazao ya biashara umekuwa ukiongezeka kuanzia msimu wa mwaka 2005/2006 hadi msimu wa mwaka 2010/2011 kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na 15: Uzalishaji wa Mazao ya Biashara Kimsimu**

<b>Mazao ya Biashara</b>	<b>2005/2006</b>	<b>2006/2007</b>	<b>2007/2008</b>	<b>2008/2009</b>	<b>2009/2010</b>	<b>2010/2011</b>
Korosho	48000	54008	62022	50387	49806	86058
Ufuta	5208	19693	16000	4177	19005	23799
Soya	14	100	10	10	160	160
Karanga	21427	20489	22460	14054	40211	43886
Nazi	-	27331	6841	7885	-	6734

- **Pembejeo za Kilimo**

- ✓ Mwamko wa matumizi ya dawa ya kupulizia mikorosho umeongezeka kutoka tani 2,653 kwa msimu wa mwaka 2005/2006 hadi kufikia tani 102,000 kwa mwaka 2010/2011.

**Jedwali Na.16: Pembejeo za Kilimo**

<b>Aina ya Dawa</b>	<b>2005/2006</b>	<b>2006/2007</b>	<b>2007/2008</b>	<b>2008/2009</b>	<b>2009/2010</b>	<b>2010/2011</b>
Unga	2,653	18,412	26,189	76,864	90,200	102,000
Maji	46,183	53,519	56,189	345,082	250,083	604,906

- **Kilimo cha Umwagiliaji**

- ✓ Katika msimu wa 2003/2004 Mkoa ulikuwa na hekta 1,866 zilitumika kwa kilimo cha umwagiliaji. Hadi kufikia msimu wa 2009/2010 eneo linalotumika ni hekta 2,969 sawa na ongezeko la Ha 1,103 (62.9%).

- ✓ Skimu za umwagiliaji zimeongezeka kutoka skimu 5 mwaka 2003/2004 hadi 15 kwa mwaka 2010/2011. Kati ya hizo skimu 9 zimeendelezwa kwa kujengewa miundo mbinu ya umwagiliaji.

**Picha Na: 7. Skimu ya Umwagiliaji Ndanda.**



- ✓ Uzalishaji wa mpunga umeongezeka kama takwimu zinavyoonyesha kwenye Jedwali Na; 12.
- ✓ Wakulima 2300 na Wagani Jamii 400 wamepata mafunzo ya muda mfupi katika Chuo cha Kilimo Mtwara (MATI) mwaka 2009/2010.

- **Mifugo**

Kutokana na kuongezeka kwa mwamko wa matumizi ya mazao ya mifugo idadi ya baadhi mifugo imeongezeka huku mingine ikipungua kama ifuatavyo:-

**Jedwali Na 17. Idadi ya Mifugo**

<b>Aina ya Mifugo</b>	<b>Mwaka 1996</b>	<b>Mwaka 2011</b>
Ng'ombe	19,700	24,294

Mbuzi/Kondoo	16,400	590,152
Nguruwe	6,000	9,420
Kuku/Bata/Kanga	3,200,000	1,297,730
<b>JUMLA</b>	<b>3,239,100</b>	<b>1,913,118</b>

- ✓ Wataalamu 12 wa mifugo wamepata mafunzo ya uhamilishaji (Artificial Insemination) mwaka 2009/2010.
- ✓ Kusambazwa kwa majogoo 726 ya kisasa katika Halmashauri zote sita (6).

### 7.2.2 Viwanda/Ushirika

Hadi Uhuru unapatikana Mkoa wa Mtwara haukuwa na viwanda, kufikia mwaka 2011 Mkoa una viwanda ifuatavyo;

- **Viwanda vya kubangua Korosho:**

- ✓ OLAM chenye uwezo wa kubangua Korosho tani 4,800 kwa mwaka na kuajiri watu 4,000
- ✓ Annar Cashew Factory chenye uwezo wa kuajiri wafanyakazi 300
- ✓ Agro Focus chenye uwezo wa kuajiri wafanyakazi 200
- ✓ Sannol Cashew Factory chenye uwezo wa kuajiri wafanyakazi 250
- ✓ Kitama Farmers Group chenye uwezo wa kuajiri wafanyakazi 75
- ✓ Masasi High Quality Farmers Products chenye uwezo wa kuajiri wafanyakazi 50
- ✓ Viwanda vidogo vidogo vya River Valley Food (RVF)
- ✓ Cashewnut Company 2005 (CC 2005)

- **Viwanda vya Maji**

- ✓ Ndanda Springs
- ✓ Ndanda IMRAN

- ✓ Makonde Pure Drinking Water

**Picha Na.8: Kiwanda Cha Maji Ndanda.**



### 7.2.3 Misitu/Nyuki/Mazingira

- ✓ **Upandaji Miti**

Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2005 hadi 2011 Mkoa ulikusudia kupanda miti 48,000,000 na hadi kufikia mwaka 2011 miti 22,700,678 imepandwa kama inavyoonekana katika Jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na. 18: Upandaji Miti**

Mwaka	Lengo	Utekelezaji	Asilimia ya lengo	Eneo (Ha)
2005/2006	6,000,000	2,435,000	40.5	1429.4
2006/2007	6,000,000	3,083,400	51.4	1813.8
2007/2008	9,000,000	3,600,000	40.0	2117.6
2008/2009	9,000,000	4,200,444	46.7	2413.8
2009/2010	9,000,000	4,414,022	49.3	2608.7
2010/2011	9,000,000	4,967,812	54.1	3863.4
<b>JUMLA</b>	<b>48,000,000</b>	<b>22,700,678</b>	<b>322</b>	<b>14246.7</b>

- ✓ **Uvunaji wa Misitu**

Mwaka 2005/2006 Mkoa umekusanya shilingi 49,697,905 kutokana na mazao ya misitu. Hadi mwaka 2010/2011 makusanyo ya mapato yalifikia shilingi 111,426,803 sawa na ongezeko la shilingi 61,728,898 (44%). Mchanganuo wa ukusanyaji mapato ya Serikali kutokana na mazao ya misitu ni kama ifuatavyo:-

**Jedwali Na 19: Ukusanyaji Mapato**

<b>Mwaka</b>	<b>Serikali Kuu</b>	<b>MSM</b>	<b>JUMLA</b>
2005/2006	48,508,082	1,189,123	<b>49,697,905</b>
2006/2007	54,395,150	5,439,515	<b>59,834,665</b>
2007/2008	113,860,232	6,542,000	<b>120,342,232</b>
2008/2009	146,918,935	10,672,000	<b>157,990,935</b>
2009/2010	141,936,000	18,079,566	<b>160,015,566</b>
2010/2011	106,120,765	5,306,038	<b>111,426,803</b>
<b>JUMLA KUU</b>			<b>659,308,106</b>

- **Uingizaji wa mbao kutoka Nje ya Nchi.**

Mkoa umefanikiwa kukusanya shilingi 83,568,380 kutokana na mapato ya mazao ya misitu kutoka Msumbiji kama inavyoonesha katika Jedwali lifuatalo:-

**Jedwali Na.20: Mapato ya Mauzo ya Mbao Kutoka Nje.**

<b>Mwaka</b>	<b>Idadi ya Mbao</b>	<b>Ujazo m3</b>	<b>Thamani</b>
2007/2008	85,330	1222.4	3,056,000
2008/2009	225,500	8498.01	21,245,250
2009/2010	329,482	9440.54	23,601,365
2010/2011	543,550	14386.306	35,665,765
<b>JUMLA KUU</b>			<b>83,568,380</b>

- ✓ Kuongezeka kwa ukusanyaji wa maduhuli kutoka shilingi 50,000,000 mwaka 2000/2001 hadi shilingi 200,000,000 mwaka 2010/2011.
- ✓ Kuanzishwa kwa chama cha wafuga nyuki Tandahimba (Tandahimba Bee Keepers Association) na kuwezesha kwa kupewa mkopo wa Benki ya CRDB

zaidi ya shilingi 75,000,000 kwa ajili ya mafunzo, zana za ufugaji na mavazi ya kujikinga.

#### **7.2.4 Uvuvi**

- ✓ Mavuno ya samaki yameongezeka kutoka tani 88,225 mwaka 1995 hadi tani 191,714 mwaka 2004 sawa na ongezeko la tani 103,489.
  
- ✓ Kuanzia mwaka 1995 mpaka 2011 jumla ya shilingi 839,041,821 zilipatikana kutokana na mauzo ya samaki.

#### **7.2.5 Wanyamapori**

- ✓ Elimu ya Uhifadhi wa wanyamapori imetolewa kwa Wananchi na Askari wa wanyamapori wa Vijiji (Village Game Scout)
  
- ✓ Wanyama wakali na waharibifu waliojitokeza sehemu mbalimbali mkoani Mtwara wamedhibitiwa ambapo wanyama kama Simba, Mamba na Tembo waliuawa.

#### **7.2.6. Barabara**

Wakati Tanzania inapata uhuru barabara ya Mtwara –Dar (Mtwara- Mtegu 41.27) km 575 ilikuwa ya kiwango cha vumbi ambayo iliwafanya wananchi kutumia wastani wa siku tano hadi saba kufika Dar- Es- Salaam. Mpaka kufikia mwaka 2003 barabara hiyo ilijengwa kwa kiwango cha lami. Pia barabara nyingine muhimu zinazounganisha Mkoa wa Mtwara na Mikoa mingine zimejengwa katika viwango mbalimbali mfano barabara ya Mangaka-Mtambaswala na barabara ya Masasi-Lumesule (Ruvuma Border) ambayo bado iko kwenye matengenezo.



Baada ya Uhuru hakukuwa na daraja ambalo lingeweza kutumiwa na wananchi wa Mtwara kuvuka Mto Ruvuma kwenda Msumbiji. Wananchi walitumia Mitumbwi kwa ajili ya kuvuka upande wa pili, na kusababisha kupoteza maisha kwa watu wengi kutokana na kuliwa na mamba na viboko.

Ujenzi wa daraja la umoja lenye urefu wa mita 720 linalounganisha Tanzania kupitia Wilaya ya Nanyumbu Mkoa wa Mtwara na kaskazini mwa Msumbiji kupitia Wilaya ya Mueda Jimbo la Cabo Delgado, kukamilika kwa daraja hili kumerahisisha mawasiliano kati ya Mkoa wa Mtwara na Msumbiji pamoja na Nchi nyingine kusini mwa Afrika.

Jedwali hapo chini linaonesha mafanikio katika sekta ya Barabara hadi sasa

**Jedwali Na. 21: Mafanikio ya Sekta ya Barabara**

<b>Kiwango cha Barabara</b>	<b>Mwaka 1996</b>	<b>Mwaka 2011</b>
<ul style="list-style-type: none"> <li>• Lami</li> </ul>	km 185	388.66
<ul style="list-style-type: none"> <li>• Changarawe/Udongo</li> </ul>	km 5461	835.84

## **8. CHANGAMOTO**

### **8.1 Elimu**

Ongezeko la Uandikishaji wa wanafunzi katika shule za Awali, Msingi na Sekondari limesababisha ongezeko la mahitaji ya miundombinu, samani, rasilimali watu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Mahitaji yote haya yamesababisha kuwepo na changamoto zifuatazo:

- ✓ Upungufu wa walimu hasa wa masomo ya Sayansi na Hisabati, vyumba vya madarasa, na nyumba za walimu katika shule za Msingi na Sekondari kama jedwali linavyoonesha hapa chini:

**Jedwali Na 22: Upungufu wa Miundombinu ya Elimu Mwaka 2011.**

<b>Shule</b>	<b>Vyumba vya madarasa</b>	<b>Nyumba za walimu</b>	<b>Madawati/viti</b>	<b>Walimu</b>
Msingi	2,723	5,595	40,532	2,265
Sekondari	558	1,716	17,529	1,914

- ✓ Uhaba wa vitendea kazi kama vile vitabu vya kiada, ziada na rejea
- ✓ Wazazi/walezi kutowajibika katika kutoa huduma stahili na kutofuatilia maendeleo ya watoto wao na hivyo kuwa chanzo cha utoro, mimba na ukosefu wa chakula shuleni.

### **8.2 Afya**

- ✓ Upungufu mkubwa wa watumishi wa kada mbalimbali katika Sekta ya Afya unaosababishwa na waajiriwa wanaopangiwa vituo vya kazi kutoripoti vituoni mwao na kuacha kazi kutokana na maslahi hafifu. Mahitaji ya mkoa ni watumishi 2,268, waliopo 1,298 na pungufu ni watumishi 970.
- ✓ Kukosekana kwa baadhi ya huduma muhimu kama X-Ray, Maabara na madawa inayosababishwa na ufinyu wa fedha za kununulia madawa kutoka serikali kuu katika baadhi ya hospitali, vituo vya afya na zahanati.
- ✓ Uhaba wa nyumba za watumishi.
- ✓ Uhaba wa vituo vya kutolea huduma za afya.
- ✓ Kukosekana kwa baadhi ya vifaa na madawa katika bohari ya madawa (MSD).

### **8.3 Mapambano dhidi ya UKIMWI**

- ✓ Baadhi ya vituo vya huduma za afya kukosa mahali pa uhakika pa kuhifadhia dawa. Miundombinu hafifu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. (Majengo, vifaa vya kutolea huduma na usafiri)

- ✓ Upungufu wa watumishi katika Sekta ya Afya
- ✓ Kamati za Kudhibiti UKIMWI hasa katika ngazi ya kata , vijiji na mitaa hazikutani kwa mujibu wa kalenda za vikao kutokana na wajumbe kukosa motisha , tofauti na vikao vya Halmashauri (CMAC) ambapo wajumbe hupewa posho.
- ✓ Ufinyu wa bajeti unachangia kutofanyika kwa vikao vya mapitio ya utekelezaji wa shughuli za mapambano dhidi ya UKIMWI katika Halmashauri za wilaya/Manispaa na Mkoa.

#### **8.4 Huduma za ustawi wa jamii.**

- ✓ Uhaba wa Maafisa Ustawi wa Jamii
- ✓ Kutohuwishwa mara kwa mara kwa takwimu za watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi
- ✓ Uhana wa vitendea kazi, unaosababisha Maafisa Ustawi kutotekeleza kazi zao kwa mujibu wa taratibu za kitaaluma
- ✓ Wilaya moja ya Nanyumbu haijafungua rasmi Ofisi ya Wilaya

#### **8.5 Maendeleo ya vijana**

- ✓ Kukosekana ajira kwa vijana
- ✓ Urejeshaji mdogo wa Mikopo kutoka katika Mfuko wa Vijana
- ✓ Upungufu wa watumishi wa kada ya Maendeleo ya Vijana katika Halmashauri
- ✓ Upungufu wa vitendea kazi

- ✓ Uchache wa Asasi zisizokuwa za Kiserikali zinazojishughulisha na masuala ya Maendeleo ya vijana
- ✓ Ukosefu wa mitaji na umiliki wa rasilimali nyingine kama ardhi kwa vijana
- ✓ Ukosefu wa elimu ya Stadi za maisha kwa vijana
- ✓ Vijana kukosa moyo wa kujitolea na kuwajibika
- ✓ Mitandao ya vijana kukosa washauri, elimu, mafunzo na fedha.

### **8.6 Michezo na Utamaduni.**

- ✓ Uhaba wa Maafisa Michezo katika Halmashauri
- ✓ Jamii kuwa na uelewa mdogo wa elimu ya michezo kwa afya.
- ✓ Uwajibikaji usioridhisha wa viongozi waliopewa dhamana ya michezo.
- ✓ Ukosefu wa Viwanja vya kisasa vya michezo mbalimbali
- ✓ Kutopatikana kwa vifaa vya michezo katika Mkoa. Hadi sasa hakuna duka /shirika linalouza vifaa vya michezo.

### **8.7 Maji**

- ✓ Uchakavu wa miundo mbinu ambao hupelekea uzalishaji wa maji kuwa hafifu.
- ✓ Ufinyu wa bajeti kutoka Serikali kuu
- ✓ Uelewa mdogo wa wananchi katika uhifadhi na ulinzi wa vyanzo vya maji.
- ✓ Kuongezeka kwa gharama za matengenezo ya vifaa na vipuri

- ✓ Ukosefu wa vifaa vya kisasa vya kufanyia tafiti za maji chini ya ardhi.
- ✓ Kupungua kwa maji chini ya ardhi kunakotokana na mabadiliko ya tabia ya nchi na uharibifu wa mazingira.

### **8.8 Madini**

- ✓ Kutofanyika kikamilifu kwa tafiti za madini mkoani Mtwara ambako kumesababisha uchimbaji mdogo wa madini.
- ✓ Uduni wa teknolojia ya utafiti na uchimbaji.

### **8.9 Misitu**

- ✓ Uvunaji holela wa mazao ya misitu.
- ✓ Uharibifu wa mazingira kama uchomaji moto hovyoo wa misitu
- ✓ Kutokuwa na mipango maalumu ya kuhifadhi misitu ya Serikali.
- ✓ Gharama kubwa za upatikanaji wa mazao ya misitu.
- ✓ Uhaba wa wafanyakazi katika idara ya misitu na nyuki katika ngazi za wilaya
- ✓ Ukosefu wa vitendea kazi

### **8.10 Uvuvi**

- ✓ Matumizi ya zana duni za uvuvi ambazo husababisha kushuka kwa mavuno ya samaki.
- ✓ Uvuvi haramu wa kutumia mabomu, sumu na nyavu zilizokatazwa kisheria (nyavu zenye matundu chini ya mm.2).
- ✓ Elimu duni ya uvuvi

- ✓ Mitaji midogo ya kununulia zana bora za uvuvi.
- ✓ Kutokuwepo na sehemu za kuhifadhia samaki (cold rooms).
- ✓ Kutoweka kwa baadhi ya mazao ya bahari kama vile Majongoo bahari.

### **8.11 Wanyamapori**

- ✓ Kuendelea kuwepo kwa ujangili wa wanyama pori
- ✓ Kuendelea kujitokeza kwa wanyama wakali na waharibifu ambao husababisha vifo na uharibifu wa mali na mazao
- ✓ Upungufu wa wataalamu
- ✓ Ufinyu wa bajeti
- ✓ Ubovu wa Miundombinu kama barabara kuyafikia maeneo ya hifadhi.

### **8.12 Kilimo**

- ✓ Ukosefu wa wakandarasi wenye ujuzi katika ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji.
- ✓ Mabadiliko ya hali ya hewa ambayo husababisha kutofikia malengo ya mavuno yaliyopangwa.
- ✓ Ongezeko la magonjwa ya mazao na wadudu waharibifu wanaoshambulia mazao yakiwa mashambani na maghalani.
- ✓ Matumizi ya moto katika kupalilia mikorosho.
- ✓ Kupanda kwa gharama za madawa
- ✓ Kuibuka kwa magonjwa mapya ya mikorosho kama Ubwiliunga
- ✓ Mabadiliko ya hali ya hewa yanasababisha mifugo kukosa malisho

- ✓ Kupanda kwa bei za madawa ya mifugo kulikosababisha baadhi ya wafugaji kushindwa kununua dawa kwa ajili ya mifugo yao.

### **8.13 Viwanda/Ushirika**

- ✓ Uendeshaji usioridhisha unasababisha baadhi ya viwanda kufa au kushindwa kufanyakazi.
- ✓ Uhaba wa watumishi
- ✓ Ukosefu wa vitendea kazi
- ✓ Elimu duni kwa wanachama wa vyama vya ushirika
- ✓ Uaminifu mdogo kwa baadhi ya watendaji katika vyama vya ushirika
- ✓ Uchache wa wanachama ukilinganisha na idadi ya wananchi
- ✓ Baadhi ya Vyama vya Ushirika vya Msingi kushindwa kujiendesha.

## **9. MATARAJIO YA MKOA WA MTFWARA MIAKA 50 IJAYO**

### **9.1 Elimu**

- ✓ Mchakato wa kufundisha na kujifunza kufanyika kwa kutumia Teknolojia ya Kompyuta.
- ✓ Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kuimarisha/kuongeza miundombinu katika shule ili kuwavutia walimu na watumishi wengine kufanya kazi katika maeneo yote ya Mkoani.
- ✓ Kuendelea kutoa Elimu kwa jamii kupitia mikutano, matangazo, vyombo vya habari ili kuongeza idadi ya wanafunzi wanaomaliza shule ambao watakuwa wakala wa kuleta mabadiliko katika jamii.

- ✓ Kuendelea kuhimiza wanaomaliza Elimu ya Msingi na Sekondari kujiunga na Vyuo vya Ufundi Stadi na Ufundi katika Vyuo vya VETA ili kupata ujuzi na Maarifa.
- ✓ Kuwa shule za Sekondari za kidato cha V-VI katika Tarafa.

## **9.2 Afya**

- ✓ Kuhakikisha kunakuwepo na watumishi wa afya wakutosha katika maeneo yote ya kutolea huduma za afya.
- ✓ Kuhakikisha maeneo yote ya huduma za afya yanakuwa na madawa ya kutosha wakati wote na kuboresha Bohari ya kuhifadhia dawa.
- ✓ Kuhakikisha kuwa huduma ya bure ya afya kwa wazee inaboreshwa na kuwa endelevu.
- ✓ Kuendelea na upanuzi wa maeneo ya kutolea huduma za afya ili kuongeza wigo wa kutoa huduma.

## **9.3 Mapambano dhidi ya Ukimwi**

- ✓ Kuunganisha kliniki za UKIMWI kwa Kutumia huduma za pamoja (kifua kikuu na UKIMWI).
- ✓ Kuhamasisha ushiriki wa sekta mbalimbali katika kuanzisha udhibiti wa UKIMWI mahala pa kazi.
- ✓ Kuhakikisha watoto wote wenye VVU wanapata huduma za madawa.
- ✓ Kusisitiza upatikanaji wa FACS Count machine katika kila hospitali.
- ✓ Halmashauri kuwezesha uendeshaji wa shughuli na vikao vya kamati za Kata na Vijiji/Mitaa ili utekelezaji wa majukumu yao uwe timilifu.



- ✓ Kuimarisha mfumo wa kupeana taarifa kati ya timu ya Mkoa, CMAC, CSOs na wadau wengine kuhusu shughuli za mapambano katika maeneo husika kupitia vikao vya tathmini katika ngazi mbalimbali.
- ✓ Kuimarisha utoaji wa elimu ya UKIMWI kwa kutumia maonesho ya sinema kwa jamii.

#### 9.4 Ustawi wa Jamii

- ✓ Kila Halmashauri kuanzisha ofisi za Ustawi wa Jamii za wilaya.
- ✓ Kila Kata kuwa na Mtumishi mwenye taaluma ya Ustawi wa Jamii
- ✓ Kuhakikisha watendaji na viongozi katika ngazi ya vijiji, vitongoji na mitaa wanapatiwa mafunzo ya **PARA SOCIAL WORKER**.
- ✓ Watoto wote wanaoishi katika mazingira hatarishi wanapatiwa huduma za msingi katika ngazi ya jamii.
- ✓ Kuhakikisha watoto wote wenye ulemavu wanapata fursa ya elimu.

#### 9.5 Maendeleo ya vijana

- ✓ Kuwa na mpango wa elimu ya ujasiriamali na stadi za maisha kwa vijana kwa ushirikiano na wadau wengine wa maendeleo mkoani Mtwara
- ✓ Kuwa na programu za kujitolea kwa vijana
- ✓ Kuwa na wataalamu wa kutosha wa sekta ya Maendeleo ya Vijana katika kila Halmashauri
- ✓ Jamii kushiriki katika programu za maendeleo ya vijana

## 9.6 Michezo na Utamaduni.

- ✓ Kutoa fursa kwa wananchi wengi zaidi kushiriki katika michezo.
- ✓ Kushirikiana na vyama vya michezo na sanaa katika kuendeleza vilabu vyote ili viweze kupanda madaraja.
- ✓ Kuanzisha michezo isiyokuwepo mkoani kama mashindano ya baiskeli na kuogelea.
- ✓ Kuwa na Viwanja vya kisasa vya michezo mbalimbali.

## 9.7 Maji

- ✓ Kila kaya kuwa na miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua
- ✓ Kila mahali penye chanzo cha maji kuwa na jumuiya za watumiaji maji zilizosajiliwa kwa ajili ya usimamizi na utunzaji wa mazingira.
- ✓ Jamii kushiriki katika mipango ya maendeleo ya sekta ya maji.
- ✓ Kuwa na wataalamu wa kutosha wa sekta ya maji

## 9.8 Kilimo

- ✓ Kuwa na aina bora za Mikorosho zitakazokuwa na uwezo wa kuhimili magonjwa na kuongeza uzalishaji.
- ✓ Kuwa na mazao mengine ya biashara.
- ✓ Kununua pembejeo kwa bei nafuu kutoka kwenye vyanzo vya uzalishaji badala ya kuwatumia mawakala.
- ✓ Kuwa na mifugo inayostahimili magonjwa (Borani)
- ✓ Wananchi kuwa na uelewa kuhusu umuhimu wa chanjo ya mifugo

### 9.9 Viwanda/Ushirika

- ✓ Kuimarika kwa ubia kati ya wamiliki wa viwanda na wakulima ili kufanikisha zoezi la usindikaji wa mazao.
- ✓ Kuwa na watumishi wakutosha na kuwa na vitendea kazi
- ✓ Watendaji na wanachama kuwa na stadi za ujasiriamali, sheria na kanuni za vyama vya ushirika.
- ✓ Kuwa na vyama vya Ushirika vinavyojiendesha kibiashara.
- ✓ Kuongezeka kwa wigo wa vyama vya ushirika
- ✓ Vyama vyote vya ushirika kutumia teknolojia ya kisasa

### 9.10 Misitu/Nyuki/Mazingira

- ✓ Kuwa na usimamizi shirikishi wa misitu, mazingira na vyanzo vya maji.
- ✓ Jamii kuwa na elimu ya ufugaji nyuki, uvunaji asali, uchakachuaaji na utunzaji asali kwa ajili ya kuongeza thamani.
- ✓ Kufanikisha utekelezaji wa Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa ya Ukaa (MKUHUMI)

### 9.11 Uvuvi

- ✓ Uvuvi haramu kudhibitiwa kwa kuongeza nguvu kwenye kufanya doria.
- ✓ Kudhibitiwa kwa uvunaji wa mazao ya bahari.
- ✓ Kuwa na miradi ya mabwawa ya samaki katika ngazi ya jamii.
- ✓ Kuwa na zana za bora za kisasa za uvunaji wa samaki.
- ✓ Kuwa na wawekezaji wa kutosha kwenye sekta ya uvuvi.

- ✓ Kuwa na SACCOS za wavuvi

#### 9.12 Wanyamapori

- ✓ Kuwa na mapori ya wanyama yanayomilikiwa na kuongozwa na jamii (Wildlife Management Areas).
- ✓ Kuendelea kudhibiti wanyama wakali na waharibifu
- ✓ Kudhibitiwa kwa ujangili na usafirishaji wa nyara za serikali

### 10. HITIMISHO

Mafanikio yaliyopatikana kisiasa, kiuchumi, kiulinzi, kijamii na kiteknolojia ni matunda ya ushirikiano mzuri uliopo baina ya Viongozi mbalimbali Mkoani Mtwara, Vyama vya Siasa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wataalam, Watendaji mbalimbali na wananchi kwa ujumla. Ni matarajio ya Uongozi wa Mkoa kuwa ushirikiano huo utakuwa endelevu kwa maslahi ya wananchi wa Mkoa wa Mtwara na Taifa kwa ujumla kwa miaka 50 ijayo.

***‘TUMETHUBUTU, TUMEWEZA NA TUNASONGA MBELE’***